# DAWASA YETU

Jarida la Habari, Huduma na Miradi

Toleo namba 12

Julai- Desemba 2025



# Waziri Mkuu atoa Suluhu Huduma ya Maji Dar na Pwani

# BODI YA WAKURUGENZI



**Mhandisi Romanus Attilio Mwang'ingo**
Mwenyekiti wa Bodi



**Abbas Zuberi Mtemvu**
Makamu Mwenyekiti wa Bodi




**Prof. Preksedis Ndomba**
Mjumbe wa Bodi



**Abdul Rajab Mhinte**
Mjumbe wa Bodi



**Pili Hassan Mnyema**
Mjumbe wa Bodi



**Mhandisi Nixon Sanga**
Mjumbe wa Bodi



**Mhandisi Elizabeth Kingu**
Mjumbe wa Bodi



**Elihuruma Mabelya**
Mjumbe wa Bodi



**Meya Songolo Mnyonge**
Mjumbe wa Bodi




**Wakili Onesmo Mpinzile**
Mjumbe wa Bodi




**Mhandisi Mkama Bwire**
Katibu wa Bodi


# MENEJIMENTI




**Mhandisi Mkama Bwire**
Afisa Mtendaji Mkuu




**Mhandisi Ramadhani Mtindasi**
Mkurugenzi wa Miradi na Uwekezaji




**Mhandisi Lydia Ndibalema**
Mkurugenzi Huduma za Usafi wa Mazingira




**Florence Yamat**
Mkurugenzi wa Huduma za Sheria



**Paul Sulley**
Mkurugenzi wa Mipango Tathimini na Ufuatiliaji




**CPA (T) Rithamary Lwabulinda**
Mkurugenzi wa Huduma kwa Wateja




**Mhandisi Leonard Msenyele**
Mkurugenzi wa Uzalishaji na Usambazaji Maji




**Mhandisi Modesta Mushi**
Mkuu wa Kitengo cha Mazingira




**CPA (T) Rosemary Lyamuya**
Mkurugenzi wa Ukaguzi wa Ndani




**Mhandisi Christian Christopher**
Mkuu wa Kitengo cha Udhibiti Ubora




**Bernadetha Mwabusila**
Kaimu Mkurugenzi Rasilimali Watu na Utawala




**Emily Ntangwa**
Mkurugenzi wa Huduma za Manunuzi




**CPA (T) Grace Kasongwa**
Kaimu Mkurugenzi wa Fedha



**Everlasting Lyaro**
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano



**Charles Kayuza**
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA



**Mhandisi Tyson Mkindi**
Msimamizi wa Kitengo cha udhibiti upotevu wa Maji

# Bodi ya Wahariri




01 **Mhandisi Mkama Bwire:** Mwenyekiti
02 **Everlasting Lyaro:** Mhariri Mkuu
03 **Joseph Mkonyi:** Mjumbe
04 **Jamal Chuma:** Mjumbe
05 **Crispin Gerald:** Mjumbe
06 **Humphrey Jimmy:** Mjumbe
07 **Fredrick Mshiu:** Mjumbe
08 **Irene Thompson:** Mjumbe
09 **Nelson Shoo:** Mjumbe
10 **Hashura Kamugisha:** Mjumbe
11 **Neema Manyama:** Mjumbe
12 **Jamil Bakari:** Mjumbe
13 **Prisca Makenya:** Mjumbe



**Anuani:** Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA)
Barabara ya Chuo Kikuu, Ubungo | S.L.P 1573, Dar es Salaam, Tanzania
181 (Bila malipo) 0735 202 121 info@dawasa.go.tz www.dawasa.go.tz

# Yaliyomo
## Ndani ya Jarida


01 Upungufu wa Maji mtoni ni kutokana na Mabadiliko ya Tabianchi - Waziri Mkuu

02 Waziri Aweso aridhishwa na wingi wa Maji Ruvu Juu

08 Mhandisi Bwire asimamia ratiba ya mgao wa Maji, akagua Huduma Kinondoni

11 DAWASA yaingia mtaani kufuatilia uimarikaji wa huduma

21 Ujenzi Bwawa la Kidunda wafikia asilimia 40, kukabili Mabadiliko ya Tabianchi

37 DAWASA yaimarisha usalama wa Huduma za Maji










# Upungufu wa Maji mtoni ni kutokana na Mabadiliko ya Tabianchi – Waziri Mkuu





Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Mwigulu Nchemba amesema kuwa changamoto ya maji iliyotokea hivi karibuni siyo uzembe wa mtu bali ni kutokana na mabadiliko ya tabianchi yanayoathiri nchi yoyote.

Amesema kuwa mabadiliko ya tabianchi ni jambo mtambuka linaloikumba nchi yoyote Duniani, na imekuwa ikileta athari mbalimbali ikiwemo ukame kama ilivyotokea hapa.

"Pamoja na changamoto hii nipende kuwajulisha wananchi kuwa Serikali haijalala na imeliona suala hili na tayari hatua madhubuti za kukabiliana na hali hii kwa kipindi kijacho zilishachukuliwa ili kuepusha kutokea kwa changamoto ya namna hii," amesema Mhe. Nchemba alipokuwa kwenye ziara ya kukagua hali ya maji katika Mtambo wa Ruvu Chini.

Hatua hizo ni pamoja na ujenzi wa mradi wa kisasa wa Bwawa la Kidunda lenye uwezo wa kuhifadhi lita bilioni 195 za maji zitakazotumika kwa kipindi chote cha ukame.

Mhe. Dkt. Nchemba ameongeza kuwa Serikali imeongeza nguvu katika matumizi ya vyanzo vya maji ya ardhini ikiwemo visima virefu vilivyochimbwa Kigamboni, ambavyo vilisaidia kukuza upatikanaji wa maji, na pia tunakusudia kuongeza wigo wa vyanzo hivyo ili viweze kutoa huduma kwa ukubwa.

"Niwahakikishie wananchi kazi iliyofanyika katika Mto Ruvu na kwenye Mtambo wa Ruvu Chini ya kufuatilia maji ni kazi makini na imesaidia kwa kiasi kikubwa maji kurejea Mtoni, hivyo niwatoe hofu wananchi hali ya maji kwa sasa iko salama," amesema Mhe. Nchemba.

Kwa upande wake Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso ameishukuru Serikali kwa kuwezesha utekelezaji wa mradi wa visima Kimbiji ambao umesaidia kutoa maji ya visima na kulisha wakazi wa maeneo ya katikati mwa Jiji.

Pia niwapongeze sana Watumishi, Bodi ya Wakurugenzi pamoja na Menejimenti ya DAWASA kwa kujitoa kwao kwa kipindi chote cha changamoto hii.

Naye Afisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA Mhandisi Mkama Bwire amesema kupungua kwa maji Mtoni kunatokana na mabadiliko ya hali ya hewa, yaliyosababisha mvua za masika kuchelewa kunyesha, pamoja na matumizi ya Mto kuzidiwa.

"Hivyo DAWASA kwa kushirikiana na Wizara na Bonde la Wami tulifanya doria ili kuondoa wakulima katika Mto, lakini pia tulitumia vyanzo vya maji ya visima vya Kigamboni vilivyosaidia kuongeza upatikanaji wa maji kwa wananchi wa kati ya mji," ameeleza Mhandisi Bwire.

Mpango uliopo wa DAWASA kwa kushirikiana na Wizara ya Maji, ni kutekeleza awamu ya pili ya mradi wa visima Kimbiji - Mpera ili kuongeza upatikanaji wa maji kwa wananchi.

# Aweso aridhishwa na wingi wa Maji Ruvu Juu

Waziri wa maji Mhe.Jumaa Aweso (Mb), amekagua na kujiridhisha na wingi wa Maji yanayoingia katika Mtambo wa Maji Maji Ruvu Juu uliopo Wilaya ya Kibaha Mkoani Pwani ikiwa ni ishara ya kuendelea kuimarika kwa huduma ya Maji.

Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amesema hatua hiyo ni jitihada zinazoendelea kutekelezwa na Serikali kupitia Wizara ya Maji na Taasisi za DAWASA na Bonde la Wami Ruvu za kuhakikisha inapambana na upungufu wa huduma ya maji iliyojitokeza katika mikoa ya Dar Es Salaam na Pwani.

"Nimeona kazi inayoendelea niseme kwa dhati nimefarijika na inanipa imani kubwa kwamba tutavuka salama katika kipindi hiki cha mpito, niwapongeze watu wa DAWASA, Bonde la Wami Ruvu, vyombo vya ulinzi na Usalama pamoja na wadau wote wanaoshiriki kazi hii kuhakikisha inakamilika kwa wakati" ameeleza Waziri Aweso.

Mheshimiwa Aweso ameeleza kuwa maendeleo ya kazi hii ni hatua muhimu katika jitihada za kuwapatia huduma endelevu ya maji wananchi wa Dar Es Salaam na Pwani na kuendelea kuwaasa Wananchi kutumia maji kwa uangalifu na kuwa na desturi ya kuwa na



vyombo vya kuhifadhi Maji.

"Tumepokea habari njema kutoka kwa wenzetu wa Mamlaka ya hali ya hewa kuwa mvua zinaanza kunyesha, na tayari katika maeneo ya Morogoro mvua imenyesha siku ya Jana, nina imani kubwa tutavuka salama kipindi hiki cha mpito na hali kurejea sawa.

Katika kipindi hiki tutahakikisha maji yanayopatikana yanagawanywa kwa usawa kwa kila Mwananchi" amesisitiza Mheshimiwa Aweso.






# RC Chalamila ataka mikakati ya haraka kuboresha Huduma ya Maji Dar es salaam

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Albert Chalamila ameiagiza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kufuatilia hali ya upatikanaji wa huduma ya majisafi katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na kuweka mikakati ya haraka ya kuboresha huduma hiyo.

Mheshimiwa Chalamila ametoa maelekezo hayo wakati wa kikao kifupi na Watendaji wa DAWASA cha kufanya tathmini ya hali ya upatikanaji wa maji kwa kubaini maeneo yenye changamoto ya maji kwa muda mrefu ili kutatua na kuboresha huduma ya maji.

Amesema kuwa Serikali imefanya uwekezaji mkubwa katika sekta ya maji kwa kutekeleza miradi mikubwa ya maji ikiwemo mradi wa maji Dar es Salaam ya Kusini (Bangulo) ambao umekamilika na kuanza kutoa huduma katika maeneo ya Segerea, Kinyerezi, Kibamba na Ubungo ambayo awali imekuwa na changamoto ya maji kwa muda mrefu.

''Nikiri kweli kuna maeneo mengi ya Dar es Salaam ambayo yanakabiliwa na upatikanaji mdogo wa maji, nitoe rai kwa wananchi wa maeneo hayo kuwa na subira wakati Serikali kupitia DAWASA ikichukua hatua za haraka za kuhakikisha huduma inaboreshwa.'' amesema Mhe. Chalamila.

Amesema kuwa hatua nyingine ambayo Serikali inachukua ni pamoja na matumizi ya maji ya visima zaidi ya 190 vilivyopo kwenye maeneo mbalimbali Dar es Salaam na tayari DAWASA imeanza haraka kutumia visima hivyo kwa lengo la kuongeza kasi ya upatikanaji wa maji.

Kwa upande wake Afisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA Mhandisi Mkama Bwire amesema kuwa Mamlaka imepokea maelekezo kutoka kwa Mkuu wa Mkoa na kazi kubwa inaendelea kutekelezwa na Mamlaka kwa lengo la kuboresha huduma.

Amesema kuwa kwa sasa katika eneo la huduma la DAWASA mahitaji ya maji kwa wananchi yameongezeka kwa kiasi kikubwa hadi kufikia mita za ujazo 685,677 kwa siku kutokana na ongezeko la watu mjini, ilihali uzalishaji wa maji kwa siku ukiwa mita za ujazo 534,600.

Amesema kuwa jitihada kubwa zimefanyika na Serikali kwa lengo la kuimarisha upatikanaji mkubwa wa huduma ikiwemo utekelezaji wa mradi wa maji Bangulo unaotoa huduma kwa wakazi wa Segerea, Ukonga, Kisarawe, na maeneo ya Kinyerezi yaliyokuwa na changamoto ya huduma hapo awali.

# RC Kunenge awatoa hofu Wananchi upatikanaji wa Maji Mto Ruvu

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mheshimiwa Abubakary Kunenge amewaondoa hofu wananchi wa mikoa ya Dar es Salaam na Pwani juu ya upatikanaji wa maji katika chanzo cha mto Ruvu.

Aidha ametoa wito kwa wananchi wanaotumia mto huo kwa matumizi mbalimbali kinyume na sheria kuacha mara moja ili kuepuka kuchukuliwa hatua za kisheria.

Mheshimiwa Kunenge ameyasema hayo katika ziara yake ya kukagua hali ya maji na uzalishaji katika mitambo ya maji Ruvu juu na Chini Mkoa wa Pwani.

"Ni kweli hali ya wingi wa maji mtoni imepungua hasa upande huu wa Ruvu chini, na hii ni kutokana na kuongezeka kwa joto pamoja na kuchelewa kwa mvua, ila niwatoe wasiwasi wananchi kuwa hatupo kwenye hali inayoweza kuleta taharuki na maji yanaendelea kuzalishwa na Kusambazwa kwa wateja," amesema Mheshimiwa Kunenge.

Kunenge amesema pamoja na jitihada na Mipango ya Wizara ya maji kupitia DAWASA Kuongeza uzalishaji wa maji katika mitambo yake, wapo wananchi wanaohujumu jitihada izo kwa maksudi kwa kutumia maji bila kufuata utaratibu hali inayoleta changamoto na kupunguza wingi wa maji mtoni.

"Kwanzia kipindi hiki maji yaliyopo mtoni ni kwajili ya matumizi ya binadamu tu, tunafahamu Kuna wanaoendesha shughuli za kilimo pembezoni mwa mto bila kibali, waache mara moja na tutawafuatilia wote kupitia kamati yetu ya mikoa mitatu hii ya Dar es Salaam, Pwani na Morogoro ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yao," amesema Mhe.Kunenge.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Mwajuma Waziri amewataka Bonde la maji Wami-Ruvu kwa kushirikiana na DAWASA kufanya jitihada za haraka na upesi kuboresha maeneo yenye changamoto katika mto Ruvu yanayopelekea maji kupotea na kupunguza wingi wa maji mtoni ili wananchi wananchi waendelee kupata huduma ya maji yenye uhakika.





# Rais Samia atambulika kuwa kinara katika huduma ya Maji kwa Tuzo ya juu ya kimataifa

**Tuzo imetolewa wakati wa Mkutano wa Kilele wa Uwekezaji katika Sekta ya Maji wa AU-AIP 2025, ulioanza jijini Cape Town, Afrika Kusini, na unatarajiwa kumalizika tarehe 15 Agosti 2025.**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan ametunukiwa Tuzo ya Rais ya Kimataifa ya Wabunifu wa Mabadiliko katika Sekta ya Maji 2025 (Presidential Global Water Changemakers Award 2025), heshima kubwa inayotolewa na taasisi ya maji duniani, (Global Water Partnership) kwa ushirikiano na Umoja wa Afrika.

Tuzo hiyo imetolewa rasmi na Rais Duma Boko wa Jamhuri ya Botswana, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Tuzo za Rais za Kimataifa za Wabunifu wa Mabadiliko katika Sekta ya Maji 2025, ambapo kwa niaba ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, tuzo ilipokelewa na Balozi James Bwana, Balozi wa Tanzania nchini Afrika Kusini.

Tuzo imetolewa wakati wa Mkutano wa Kilele wa Uwekezaji katika Sekta ya Maji wa AU-AIP 2025, ulioanza jijini Cape Town, Afrika Kusini, na unatarajiwa kumalizika tarehe 15 Agosti 2025.

Global Water Partnership imetambua uongozi bora na jitihada za mageuzi za Rais Samia katika sekta ya maji, ikiwemo uwekezaji mkubwa katika miundombinu ya maji, upanuzi wa huduma ya maji safi kote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na mikakati bunifu ya ufadhili kama vile hati fungani ya Kijani (Green Bond) lililotolewa na Mamlaka ya Maji ya Tanga chini ya Wizara ya Maji.



# Ujenzi Bwawa la Kidunda wafikia asilimia 40, kukabili Mabadiliko ya Tabianchi



Waziri wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Aweso (Mb) amesema kukamilika kwa ujenzi wa Bwawa la Maji Kidunda kutasaidia kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi ikiwemo ukame wa muda mrefu utakaomaliza tatizo la maji jijini Dar es Salaam.

Aweso amesema hayo leo Jumanne, tarehe 16 Desemba mwaka huu katika ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa bwala hilo uliofikia asilimia 40 akiambatana na Wakuu wa Mikoa ya Dar es Salaam, Albert Chalamila, Abubakar Kunenge wa Pwani na Adam Malima wa Morogoro ambayo itanufaika na mradi huo.

"Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kutupatia fedha zaidi ya Shilingi Bilioni 335 kutekeleza mradi huu wa kimkakati ambao kukamilika kwake kutamaliza changamoto ya upatikanaji wa maji hususani kipindi cha ukame," amesema Mheshimiwa Aweso.

Amewaomba wananchi kulinda vyanzo vya maji lakini pia kuwa na utaribu mzuri wa kuhifadhi maji wakati Serikali inaendelea kuboresha hali ya upatikanaji huduma ya maji nchini kote.

Aidha, Mheshimiwa Aweso amesema Serikali katika kutatua changamoto ya maji nchini kote imeanza utekelezaji wa Gridi ya Taifa ya Maji kwa kuunganisha vyanzo vya maji vyote vikubwa nchini ili wananchi wapate huduma.

Akizungumza kwa niaba ya Wakuu wa Mikoa, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Mheshimiwa Adam Malima amesema swala la utunzaji wa vyanzo vya maji lazima lichukuliwe kwa umuhimu wa hali ya juu na kwa ushirikiano wa mikoa yote mitatu ya Dar es Salaam, Pwani na Morogoro watahakikisha mto unabaki salama na kutumiwa kwa matumizi sahihi pekee.





# Serikali kutumia visima kuongeza Maji Dar na Pwani

Serikali kwa kushirikiana na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) imeainisha mkakati madhubuti wa uchimbaji wa visima vya uzalishaji maji na kufufua vilivyopo katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Dar es Salaam kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa maji kwa wananchi wote.

Mkakati huu ni mpango wa muda mfupi wa kukabiliana na changamoto hii ya upungufu wa maji katika vyanzo vya uzalishaji maji ikiwemo Mto Ruvu.

Akizungumza na waandishi wa habari Afisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA Mhandisi Mkama Bwire amesema kuwa zoezi hili limekwishaanza kwa baadhi ya maeneo ikiwemo Mwananyamala la kufufua visima na kuviingiza kwenye mfumo ili viweze kuongeza maji kwenye mfumo na wananchi wapate maji, kazi inaendelea ya kuhakikisha hali hii inakabiliwa vizuri.

Amesema kuwa pia itahusisha uchimbaji wa visima virefu vya Kimbiji Kigamboni ambavyo vitakuwa na uwezo mkubwa wa kuongeza kiasi cha maji katika mfumo wa usambazaji maji kwa wananchi.


"Tunashirikiana na Serikali kupitia Wizara ya Maji katika kutekeleza hili, na tunawasihi wananchi kuwa wasimamizi wazuri wa miundombinu hii ya maji ambayo imesogezwa katika makazi yao," ameeleza Mhandisi Bwire.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Bonde la Wami Ruvu Mhandisi Elibariki Mmasi amesema kuwa jitihada kubwa zinaendelea kutekelezwa na Serikali katika maeneo mbalimbali ikiwemo kusitisha vibali vya watumiaji wa skimu za umwagiliaji katika vyanzo vya maji ikiwemo Mto Ruvu ili kukabiliana na upungufu huu wa maji.

Ameongeza kuwa hatua nyingine ambayo imechukuliwa na inaendelea kutekelezwa ni pamoja na doria za mara kwa mara katika maeneo ya vyanzo vya maji kwa lengo la kukomesha shughuli nyingine zozote zinazoendelea kufanywa katika kingo za Mto Ruvu.

"Ametoa wito kwa wananchi wote kwa kila mtu kuwa mlinzi wa kutunza vyanzo vya maji katika maeneo yake na kuhakikisha hakuna maji yanayopotea bila sababu," amesema Mhandisi Mmasi.




DAWASA
ISO 9001:2015 Certified
Ifahamu
Huduma ya
Uondoshaji Majitaka
DAWASA
Bei zetu ni nafuu, tupigje 0735 451 879 - Popote jijini Dar es salaam tunakufikia.
KWA MAKAZI
• Lita 18,000 - Tsh 150,000/=
• Lita 9,000 - Tsh 100,000/=
• Lita 5,000 - Tsh 50,000/=
MAJENGO NA BIASHARA
• Lita 18,000 - Tsh 180,000/=
KARIBU TUKUHUDUMIE
DAWASA MOJA, NGUVU MOJA, TUNASONGA MBELE
0800110064
0735 202 121
www.dawasa.go.tz
info@dawasa.go.tz
@dawasatz

# Maunganisho mapya ya Maji Kin'gazi yashika kasi

Watendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kwa kushirikiana na viongozi wa serikali ya mtaa Kin'gazi A, Kata ya Kwembe, Wilaya ya Ubungo wamegawa vifaa vya maunganisho mapya ya maji kwa wananchi mbalimbali.

Lengo ni kuwezesha wananchi kuunganishwa moja kwa moja na mtandao wa majisafi wa mradi mkubwa wa kimkakati wa Usambazaji Maji Dar es Salaam ya Kusini (Bangulo) ambao umekamilika kwa gharama ya Shilingi 36.9 bilioni.

Vifaa ambavyo vimetolewa ni pamoja na mabomba, koki, dira za maji na vifaa vya usalama vya kuunganisha maji majumbani.

Meneja wa DAWASA – Kinyerezi, ndugu Roberts Mugabe amesema zoezi hilo linalenga kuhakikisha wananchi wanaanza kupata huduma ya majisafi kwa urahisi na kwa wakati ambapo wateja 130 tayari wamekabidhiwa vifaa vya maunganisho mapya na zoezi la kuunganisha huduma linaendelea.

"Mradi huu wa Bangulo umeleta mabadiliko makubwa kwa maeneo ya Kusini mwa Jiji la Dar es Salaam. Tunataka wananchi waanze kuona matokeo chanya kwa vitendo, na ndiyo maana tumeanza kugawa vifaa ili kuharakisha maunganisho ya maji," amesema ndugu Roberts.



Ndugu Roberts ameongeza zoezi la maunganisho ni endelevu kwani hadi sasa mkoa wa kihuduma umepokea maombi takribani 400 ambapo hadi sasa tayari wateja 130 wamekabidhiwa kwa ajili ya kuunganishwa huku taratibu zikiendelea kwa ajili ya waliobaki na wanaoendelea kuwasilisha maombi.

Kaimu Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Kin'gazi A, ndugu James Frank ameishukuru DAWASA na Wizara ya Maji kwa kuwaleta wananchi wake kwenye mstari wa mbele wa maendeleo, akibainisha kuwa maji ni kichocheo kikubwa cha afya na ustawi wa jamii.

''Kwa hili DAWASA inastahili pongezi kwa kusogeza huduma kwa wananchi, nitoe rai kwa wananchi kuendelea kufika ofisini kuomba huduma kwani sisi tuko kwa ajili ya kuwahudimia,» ameeleza ndugu James.

Mkazi wa Kin'gazi A, Jolicia Ngowi ameipongeza DAWASA kwa kutekeleza maelekezo ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kumtua mama ndoo kichwani.

''Tumehangaika na changamoto ya upatikanaji wa maji kwa muda mrefu ambapo ilitulazimu kununua maji kwa bei ghali au kuchota sehemu zisizo salama. Niwapongeze DAWASA kwani sasa napata maji baada ya kukamilisha taratibu ndani ya muda mfupi,'' amesema ndugu Jolicia.

Mradi wa usambazaji maji Dar es Salaam ya kusini (Bangulo) ni miongoni mwa miradi mikubwa ya kimkakati kitaifa inayotekelezwa kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa huduma ya majisafi kwa wananchi. Mradi huu unalenga kunufaisha majimbo matano ya uchaguzi ya Ukonga, Segerea, Ubungo, Ilala na Ubungo ambapo takribani wananchi 450,000 watanufaika na mradi huu.



# Wahujumu miundombinu ya Majitaka waonywa

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), imewataka wananchi kuwa na matumizi sahihi ya miundombinu ya majitaka, kuepuka kutupa taka ngumu katika miundombinu hiyo na kuwa wa kwanza kutoa taarifa kwa anayeihujumu.

Imesema baadhi ya watu wanaohujumu miundombinu ya majitaka kwa kuiba mifuniko ya chemba za majitaka na kusababisha taka ngumu kuingia jambo linalosababisha kuziba kwa chemba na kutiririsha hovyo majitaka mtaani.

Mamlaka imesema hatua hiyo inahatarisha afya za wananchi kwa kuleta hatari ya kutokea magonjwa ya mlipuko kama kipindipindu.

Hayo yamesemwa na Mhandisi Mbaraka Mpala kutoka DAWASA, mara baada ya kushuhudia maboresho ya miundombinu ya majitaka katika mtaa wa Sinza A ili kuongeza ufanisi wa mifumo ya majitaka katika eneo hilo.

Mhandisi Mpala amesema eneo hilo lilikabiliwa na changamoto katika mifumo ya majitaka hali iliyosababisha kuziba kwa chemba na kutiririsha majitaka mtaani, jambo ambalo kwasasa wamelifanyia kazi na hali ni shwari.

''Katika mtaa wa Sinza A, tumefanya maboresho makubwa ya chemba za majitaka kwa kuzijengea vizuri na kuweka mifuniko imara ambayo itazuia taka ngumu kuingia katika mifumo iyo na kusababisha uzibaji,'' amesema Mhandisi Mbaraka.

Naye Mkazi wa mtaa wa Sinza A, Ndugu Haji Ally amepongeza hatua hiyo kwani utiririkaji majitaka mtaani kulisababisha kuhatarisha afya za wakazi wa eneo hilo hususani watoto wadogo.

''Ni jambo jema kazi hii imefanyika, chemba hizi kuwa wazi ilipelekea baadhi ya wananchi kutupa taka ngumu katika mifumo hiyo na kusababisha kuziba, majitaka yakiririka mtaani afya za watu zinakua hatarini kupatwa na magonjwa ukizingatia tuna watoto wadogo hapa mtaani,''= amesema Haji.



# DAWASA yaingia mtaani kufuatilia uimarikaji wa huduma

Hali ya upatikanaji wa huduma ya majisafi imeendelea kuimarika katika maneno mbalimbali ya Mkoa wa Dar Es Salaam na Pwani mara baada ya kukamilika kwa matengenezo kinga ya miundombinu ya umeme yaliyodumu kwa Saa 10 na kusababisha kuzimwa kwa Mtambo wa Ruvu Juu na Ruvu Chini.

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar Es Salaam (DAWASA) imeingia mtaani kufuatilia upatikanaji na uimarikaji wa huduma, huku wakitoa wito kwa Mamlaka kuendelea kuboresha huduma kwa kutoa muda mrefu wa kuhifadhi maji pindi wanapoamua kufanya matengenezo.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Kambangwa, Kata ya Mwananyamala Ndugu Mkakata Abdul ameeleza kuwa wananchi walipata adha za kukosa huduma kwa siku mbili (Julai 1 na 2, 2025 ) lakini kwasasa huduma imerejea na wananchi wa eneo lake wanapata huduma ya majisafi kwa kiwango kizuri.

Hafia Ibrahim, Mkazi wa mtaa wa Kambangwa - Mwananyamala amesema kuwa huduma ya maji imerejea lakini bado baadhi ya majirani hawajapata huduma na wengine wanapata kwa msukumo mdogo.

''Tulipokea taarifa ya kukosekana kwa huduma ya maji kutoka DAWASA kwa wiki hii mapema, lakini kuanzia jana asubuhi (Julai 2,2025) huduma imerejea kwa msukumo mzuri. Wananchi tunaendelea na shughuli zetu za kila siku za kijamii na kiuchumi," alisisitiza.

Kwa upande wake, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano DAWASA, Bi Everlasting Lyaro amekiri kuwepo kwa changamoto ya ukosefu wa huduma ya maji kwa zaidi ya saa 10 kwa siku za (Jumatatu hadi Jumanne), lakini kwa sasa huduma imerejea na kuwapa uhakika wananchi wote kuwa watapata maji, huku akiwasisitiza mafundi wa Mamlaka kukesha mtaani kufuatilia huduma.

''Mamlaka ilitangaza matengenezo yaliyodumu kwa saa 10 na kufika siku ya Julai 2, tuliwasha mitambo yetu ya uzalishaji maji ya Ruvu Juu na Chini na huduma kuanza kurejea kwa wananchi. Leo tunapita mitaani kuhakikisha huduma imeimarika kwa kiasi gani na kuangalia maeneo ambayo bado yana changamoto ili tuweze kuzitatua " ameeleza Bi Lyaro.







# Wananchi Mihande wajizatiti kulinda miundombinu ya Maji

Wakati wananchi wa Kitongoji cha Mihande, eneo la Mlandizi, Mkoa wa Pwani wakijipa jukumu la kulinda miundombinu ya maji na kujitokeza kupata utaratibu wa kuunganishiwa huduma hiyo, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) imewasisitiza kulipa ankara za maji.

Wito huo umetolewa na Mwenyekiti wa Kata ya Mihande, Bi Teddy Mwaiswelo wakati wa mkutano wa wazi na wananchi na viongozi wa DAWASA uliolenga kujadili hali ya huduma ya maji pamoja na njia za kudhibiti upotevu wa maji.

Teddy amesema Serikali imetekeleza miradi mbalimbali ya majisafi kwa lengo la kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji, hivyo ni muhimu kutambua jukumu la kutunza na kulinda miundombinu ya maji liko kwenu wananchi ambao ndiyo watumiaji wakubwa.

Aidha, mwenyekiti amewasisitiza wananchi kujitokeza kwa wingi kupata maunganisho ya maji ili waweze kunufaika na uwekezaji uliofanywa na Serikali.

''Niwakumbushe wananchi miradi ya maji imeshatekelezwa na huduma imesogezwa karibu yenu, ni wakati wenu sahihi kujitokeza kupata taratibu za kuunganishiwa huduma ya maji'' amesema Teddy.

> **"Niwakumbushe wananchi miradi ya maji imeshatekelezwa na huduma imesogezwa karibu yenu, ni wakati wenu sahihikujitokeza kupata taratibu za kuunganishiwa huduma ya maji ' amesema Teddy**

Mkazi wa Kitongoji cha Mihande, Hadija Mgeni ameishukuru Serikali kwa jitihada ilizozifanya za kuwasogezea huduma ya maji katika maeneo yao akisema imewaondolea usumbufu wa kwenda kutafuta maji mbali na makazi yao.

Amewataka wakazi wenzake kuunga mkono jitihada za Serikali za kulinda miundombinu ya maji kwa pamoja ili waweze kunufaika kwa ujumla.

Naye Msimamizi wa mradi kutoka DAWASA, Mhandisi Ramadhan Mkata amesema Mamlaka kwa kushirikiana na Serikali imetekeleza miradi mingi ya kusogeza huduma ya maji karibu yao, ni wajibu wa kila mwananchi kutunza na kulinda miundombinu ya maji. Ametumia fursa hiyo kuwaita wakazi wote ambao bado hawajaunganishiwa huduma ya majisafi kufanya hivyo ili waweze kunufaika na maji.

Kwa upande wake, Afisa huduma kwa wateja, Grace Jason amewakumbusha na kusisitiza wananchi wanaodaiwa ankara kulipa mapema kabla hawajasitishiwa huduma.

# Tegeta 'A' yawatengea saa 72 kuhudumiwa



Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), Mkoa wa Kihuduma Mivumoni imetenga siku tatu za kuwasikiliza wananchi juu ya kero na kuzitafutia ufumbuzi kupitia dawati maalumu la huduma kwa wateja.

Dawati hilo limeanza Julai 24 hadi 26, 2025 ambapo wateja wa mtaa wa Tegeta A Kata ya Goba Wilaya ya Ubungo wamefika kupata huduma mbalimbali ikiwemo kutoa ushauri na mapendekezo kwa DAWASA ya namna ya kuboresha huduma za maji.

Afisa Biashara wa DAWASA Mivumoni, Shedrack Mbwambo ameelezea umuhimu wa uwepo wa dawati hilo la huduma kwa wateja kwa siku tatu (sawa na saa 72) na muitikio waliokuwa nao wananchi wa eneo hilo.

Amesema lengo kubwa la ufunguzi wa dawati hili la huduma kwa wateja ni kuwasogezea wananchi huduma karibu.

“Hapa wanaweza kupata huduma ya kuunganishiwa majisafi, kuzungumza na wateja wenye madeni ya muda mrefu, lakini pia kupokea na kusikiliza maoni ya wananchi juu ya huduma za Mamlaka kwa lengo la kuboresha zaidi,» amesema Mbwambo.

Mbwambo amesema muitikio wa wananchi kwa siku ya kwanza umekuwa mkubwa na kuwaomba wananchi waendelee kujitokeza katika madawati ya huduma kwa wateja pindi yanapofunguliwa kwani ni njia rahisi ya kukutana na kuwasikiliza.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Mtaa wa Tegeta A, Protas Luanda ameridhishwa na ufunguzi wa dawati la huduma kwa wateja akisema hatua hii ni mwanzo wa kuboresha huduma na ushirikiano kati ya wananchi na DAWASA huku akipongeza hatua hii ya Mamlaka kutoka na kuwafata wananchi kuwasikiliza.

Maria Moshi, mkazi wa mtaa wa Tegeta A, amesema kitendo cha kuwafuata wananchi na kuwasikiliza kitaongeza ukaribu kati yao na DAWASA huku akiomba utaratibu huu uwe wa mara kwa mara kuhakikisha huduma bora kwa kila mwananchi.

«Leo tumeweza kufika kwa wingi hapa ni kwa kuwa DAWASA wameshuka chini kutusikiliza huku mitaani, tunafuraha kwakuwa changamoto nyingi tulizokuja nazo hapa zimesikilizwa na kupatiwa ufumbuzi,» amesema.





# DAWASA, Wajumbe wa Matosa wajifungia kusaka suluhu ya Maji

Changamoto za upatikanaji wa maji, wizi wa mita, madeni na ulinzi wa miundombinu zimewakutanisha wajumbe wa serikali ya mtaa Matosa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) ili kuzitafutia suluhu.

Uamuzi huo wa DAWASA kupitia Mkoa wa Kihuduma Makongo ni kuitikia wito wa Waziri wa Maji, Jumaa Aweso aliyewataka kuwasikiliza wananchi juu ya kero za maji maeneo mbalimbali na kuzitatua haraha.

Kikao hicho kimeongozwa na Mwenyekiti wa serikali ya mtaa huo, Ndugu Amani Magoma na kuhudhuriwa na maafisa kutoka DAWASA pamoja na wawakilishi wa wananchi.

Lengo kuu la kikao hiki ilikuwa ni kutoa fursa kwa wananchi kupitia wajumbe wao kueleza kero, changamoto na mapendekezo kuhusu huduma ya maji ili kuyapatia suluhisho la pamoja.

Akizungumza katika kikao hicho, Magoma amesema:»Wananchi wamekuwa na malalamiko ya muda mrefu kuhusu huduma ya maji, hasa maeneo ambayo hayafikiwi na mtandao wa maji, tnashukuru sana DAWASA kwa kujitokeza kuwasikiliza wananchi wetu pamoja na kuanza kutekeleza mradi wa kusogeza mtandao wa Matosa."

Katika kikao hicho, wajumbe wameeleza kuwepo kwa maeneo kadhaa ambayo bado yanakabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa huduma ya majisafi huku wakisisitiza umuhimu wa kuhakikisha upatikanaji wa maji unaboreshwa kwa usawa na kwa wakati.

Kwa upande wake, Afisa Huduma kwa Wateja, Ndugu Christopher Sika alisema:»Tumejipanga kuhakikisha kila mteja anapata huduma bora. Tunaendelea kuboresha mifumo yetu ya kupokea taarifa kwa wakati, lakini pia Mamlaka inaendelea na utekeleza wa mradi wa kusogeza huduma kwa wananchi eneo la Matosa, hivyo tuwaondoe shaka wananchi ambao bado hawajafikiwa na huduma."

Masuala ya ulinzi wa miundombinu ya maji yalijitokeza pia, ambapo wananchi wamehimizwa kushirikiana na Mamlaka katika kulinda mabomba, matenki na vifaa vingine vya DAWASA ili kuhakikisha huduma inaendelea bila vikwazo.

Naye Ndugu Athumani Said, Mjumbe wa shina namba 8 eneo la kwa Mbilinyi amesema:»Changamoto nyingine kubwa ni wizi wa dira za maji unaosababisha uharibifu wa miundombinu. Tunawahimiza wananchi kuwa walinzi wa miundombinu hii, kwa sababu ni mali ya umma na inatugusa sisi sote."

Vilevile, kikao kimegusia suala la madeni ya maji, ambapo Mamlaka ilihamasisha wananchi kuhakikisha wanalipa madeni yao kwa wakati ili kuiwezesha mamlaka kuendelea kutoa huduma bora na kuwekeza zaidi katika miundombinu ya maji.

DAWASA imesisitiza kuwa itaendelea kuwa karibu na wananchi kwa kusikiliza na kutatua changamoto zinazojitokeza katika maeneo mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha kila kaya inapata huduma ya majisafi na salama kwa maendeleo ya jamii na afya ya umma.



# Elimu utunzaji wa miundombinu ya Maji yatolewa Kibasila

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) imetoa elimu ya umuhimu wa maji na utunzaji miundombinu ya maji kwa wanafunzi wa klabu ya mazingira shule ya sekondari Kibasila, Wilaya ya Temeke Mkoani Dar es salaam.

Lengo la elimu hii ilikuwa ni kuwaelemisha wanafunzi umuhimu wa maji na utunzaji wa miundombinu ya maji ili waweze kuwa mabalozi wazuri wa huduma hii muhimu katika jamii.

Akizungumza wakati wa kutoa elimu kwa wanafunzi wa shule hiyo, Afisa Mawasiliano kutoka DAWASA, Ndugu Prisca Makenya amesema maji ni rasilimali muhimu ambayo inahitajika kwa viumbe hai ikiwepo binadamu, mimea na wanyama, hivyo kuna ulazima wa kuyatunza na kuhakikisha yanalindwa ili yaweze kufaa kwa matumizi ya kila siku.

“Utunzaji miundombinu ya maji ni muhimu kwani unapunguza gharama zinazojitokeza wakati wa uharibifu, unasaidia upatikanaji majisafi na ya uhakika.

Miundombinu ya maji inayotumiwa na DAWASA ni pamoja na mitambo ya uzalishaji na Uzalishaji maji, mabomba, pumpu za kusukuma maji, dira za maji na viungio vyake,” amesema Ndugu Makenya.

Ndugu Makenya amesema klabu za mazingira mashuleni zimeanzishwa kwa lengo la kuwajengea vijana uwezo katika masuala ya maji na usafi wa mazingira ili wanafunzi hao wakawe chachu na mabalozi wa mabadiliko kwa jamii wanazotoka.

Wanafunzi wamejifunza njia mbalimbali ovu zinazofanywa na wanachi wasiowaaminifu kwenye miundombinu ya DAWASA ikiwa ni pamoja na kukata mabomba, wizi wa mita za maji, kurudisha usomwaji wa mita nyuma.

Kwa upande wake, Mwalimu wa Shule ya Sekondari ya Kibasila, Emmanuel Sedekia ameishukuru Mamlaka kwa kutoa elimu hii muhimu kwa wanafunzi wa shule hiyo inayowajengea uelewa wa namma nzuri ya kutunza miundombinu ya maji na hatua za kuchukua punde wanapoona wananchi wasio waaminifu wanaoharibu miundombinu.

Amewataka wanafunzi waliopatiwa elimu hiyo kuwa mabalozi wazuri wa huduma za maji katika jamii yao.

Mwanafunzi, Mashiri Bozuga aliyepata elimu hiyo, ameishukuru Mamlaka kwa kuwaelimisha na kuwasaidia kujua umuhimu wa utunzaji wa miundombinu ya maji na hatua za kuchukua pindi wanapoona uharibifu unapotokea, ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa DAWASA kupitia namba 181 ya huduma kwa wateja.

“Kwa niaba ya wenzangu, tunaahidi tutakuwa mabalozi wazuri kwa jamii kuhakikisha tunalinda miundombinu ya maji kwa manufaa ya vizazi vijavyo,” amesema Buzuga.

Klabu ya Mazingira Shule ya Kibasila ni moja ya klabu 11 za mazingira ambazo Mamlaka inazisimamia katika Mkoa wa Dar es Salaam na Pwani ili kuwajengea uwezo wa kutambua shughuli mbalimbali za Mamlaka kuhusu majisafi na usafi wa mazingira na kwenda kuwa mabalozi wazuri katika jamii.

DAWASA YETU | Julai - Desemba 2025



# Mhandisi Bwire asimamia ratiba ya mgao wa Maji, akagua Huduma Kinondoni

Afisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar Es Salaam DAWASA, Mhandisi Mkama Bwire amekagua hali ya upatikanaji huduma ya maji katika maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Kinondoni hususani Kata ya Mwananyamala na kushuhudia wananchi wakiendele kupata huduma ya maj i kama ratiba ya mgao inavyoelekeza.

"Jambo kubwa tunalosimamia ni kuhakikisha wananchi wanapata maji kulingana na ratiba inavyoelekeza, lakini zaidi kupita mitaani na kuhakikisha maji hayo yanawafikia wateja majumbani mwao" ameeleza Mhandisi Bwire

Bwire ameongeza msisitizo juu ya swala la utunzaji wa maji pale yanapotoka wananchi wawe na utamaduni wa kutunza maji lakini pia kuyatumia kwa matumizi Sahihi.

Ndugu Miriam Ally Mkazi wa Mwananyamala ametoa shukrani zake kwa DAWASA Kwakutoa taarifa ya changamoto ya upungufu wa huduma ya maji lakini zaidi kuwapatia ratiba inayoonyesha ni lini kila eneo linapata huduma ya maji.

"Tunashukuru katika eneo letu tunapata huduma ya maji mara mbili kwa wiki siku ya Jumapili na Jumatano, ingawa tunafahamu changamoto ya maji inayotukabili kwasasa, hii imesaidia kutupa utauari na ufahamu ni lini tujiandae kupata huduma ya maji, tunaomba ratiba hii izingatiwe ili pasitokee malalamiko" ameeleza Miriam



Pamoja na Ukaguzi wa huduma ya maji Elimu juu ya utunzaji wa maji na ufahamu wa ratiba ya kupata maji ilitolewa kwa wananchi mbalimbali wa eneo la Mwananyamala.

# Wanafunzi Zanaki wapewa darasa utunzaji mazingira

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) imewasisitiza wanafunzi wa Shule ya Sekondari Zanaki kuendelea kuhifadhi mazingira ili kuwawezesha kujifunza kwa ufanisi.

Zanaki iliyopo Wilaya ya Ilala jijini Dar es Salaam ni miongoni mwa shule 11 za mazingira zinazosimamiwa na kuendeshwa na DAWASA. Pamoja na mambo mengine, wanapewa elimu ya kutunza mazingira, matumizi sahihi ya maji na kulinda miundombinu ya majisafi.

Afisa Mawasiliano kutoka DAWASA, Husna Richard ameelezea umuhimu wa usafi wa mazingira shuleni na maeneo yote yanayowazunguka huku akisisitiza utunzaji sahihi wa taka shuleni katika kuhakikisha shule na mazingira yanakuwa sehemu salama ya kujifunza muda wote.

«Mazingira safi na salama huchochea hali ya kujifunza, yana mchango mkubwa katika kufanya masomo kuwa ya kuvutia zaidi na ni muhimu kwa afya ya akili kwani huepusha magonjwa katika mazingira yetu,» amesema Husna.

Mara baada ya mafunzo hayo, Mwalimu Esther Swai ambaye ni mlezi wa klabu ya mazingira shuleni hapo, ameishukuru DAWASA kwa jitihada za kuwafikia watoto wa shule za msingi na sekondari na kutoa elimu ya maji na usafi wa mazingira akiamini itakuwa chachu ya mabadiliko kwa vijana hao.

«Elimu ya maji na usafi wa mazingira ni elimu inayorithi kizazi na kizazi kwakuwa inalenga mabadiliko ya kitabia hivyo tunaishukuru sana DAWASA kwa jitihada za kutoa elimu hiyo kwa vijana wetu hakika ni hazina ya kudumu,» amesema Mwlimu Swai.

Mwanafunzi Warda Jihadhari ambaye ni mwanachama wa klabu ya maji na usafi wa Mazingira shuleni hapo ameishukuru DAWASA kuwa mlezi na kutoa nafasi ya wao kujifunza mambo mbalimbali ya maji na usafi na kuomba nafasi ya kuendelea kujifunza kwa vitendo ili kufahamu zaidi namna Mamlaka inavyoendesha shughuli zake.

«DAWASA imekuwa mlezi wa klabu yetu ya mazingira kwa muda sasa na kila mara tunajifunza vitu mbalimbali kuhusu Majisafi na Usafi wa Mazingira. Elimu ya leo imesaidia kujenga uelewa zaidi kuhusu matumizi sahihi ya maji hasa kwa sisi wanafunzi ili kuweza kupunguza gharama kubwa ya bili za maji na kuendelea kupata huduma ya maji endelevu,» amesema Jihadhari.

Mamlaka inasimamia klabu za mazingira shuleni kwa kutoa elimu mbalimbali kuhusu Majisafi na Usafi wa Mazingira, utunzaji wa miundombinu ya maji pamoja na vyanzo vya Maji na kuwaandaa wanafunzi katika rika lao kuwa mabalozi wema katika jamii katika masuala yote yanayohusu maji.





# Wakazi Msongola Juu: Maji yalitutesa, sasa 'mwa mwa mwaa'

Zaidi ya wakazi 1,000 wa Kata ya Msongola Juu, Wilaya ya Kibaha Vijijini, Mkoa wa Pwani wameishukuru Serikali kwa uamuzi wa kupeleka mradi wa kusambaza maji kwenye maeneo yao kwa lengo la kuwaondolea changamoto ya upatikanaji wa huduma.

Akizungumza mara baada ya kuanza kwa utekelezaji wa mradi huu, Afisa Mtendaji wa Kata ya Msongola Juu, Ndugu Ayubu Lugongo amesema Serikali imefanya uamuzi mzuri kwa kuwaletea huduma ya maji wakazi hao ambao walikuwa kwenye dimbwi kubwa la upatikanaji wa maji.

Amesema mradi huu unaleta furaha kubwa kwa wananchi wote kwa kuwa walikuwa wanatumia maji ya kisima ambayo siyo masafi ili waweze kukidhi mahitaji yao.

«Kwa jitihada hizi nipende kuishukuru na kuipongeza Serikali kwa kushirikiana na DAWASA na kuleta mradi huu unaotusaidia kupunguza malalamiko ya wananchi kuhusu hali ya maji,» amesema Ndugu Lugongo akisisitiza, waliteseka lakini sasa wanafurahia.

Kwa upande wake, Msimamizi wa mradi, Mhandisi Ally Migeyo amesema mradi umelenga kunufaisha wakazi wa Msongola na maeneo ya jirani walio kwenye uhaba wa maji.

Amebainisha utekelezaji wa mradi umehusisha kazi ya ulazaji wa mabomba ya inchi 4 na 3 kwa umbali wa kilomita 7.2.

Amesema mradi utanufaisha Kata hii pamoja na Kata ya Kawawa, Mlandizi kwenye vitongoji vya Sunguti, mji mwema, Upendo, Msufini na Msongola Juu.

Mhandisi ameongeza awali eneo hili halikuwa na chanzo cha huduma ya maji, wananchi



walikuwa wanapata huduma kutoka maeneo jirani, lakini kwa sasa watakwenda kunufaika na huduma ya maji moja kwa moja majumbani mwao.

Mhandisi Migeyo amewataka wananchi kulinda miundombinu ya maji ambayo Serikali imetumia gharama kubwa ya kuijenga kwa lengo la kufikisha huduma ya maji katika maeneo yao.

Mkazi wa Kata ya Msongola Ndugu Oscar Balitazari ametoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan kwa watu wa Msongola Juu, tulikuwa tunapata maji kutoka Vijiji vya jirani na maji yenyewe ni ya visima, kwa mradi huu tunashukuru sana DAWASA na usimamizi wake.



# DAWASA, Mbunge Segerea wajadili kuboresha Huduma za Maji

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), imefanya kikao kazi na Mbunge wa Jimbo la Segerea, Mhe. Agnesta Kaiza anayetokana na Chama cha Ukombozi wa Umma (Chaumma)

pamoja na Wenyeviti wa Mitaa ya Ugombolwa, Machimbo, Segerea na Migombani katika Kata ya Segerea.

Lengo lilikuwa ni changamoto za upatikanaji wa Majisafi pamoja na kutoa suluhu ya kuboresha huduma ya maji ndani ya Kata hiyo.

Katika kikao hicho, taarifa za maeneo yenye changamoto ziliwasilishwa, ikiwa ni pamoja na mitaa yenye uhaba mkubwa wa maji na uhitaji wa upanuzi wa miundombinu ambapo Mbunge pamoja na watendaji wa DAWASA walifanya ziara ya kutembelea na kukagua maeneo yenye changamoto kubwa zaidi ili kuona hali halisi na kuwezesha kuweka vipaumbele vya kuboresha utoaji wa huduma

Akizungumza katika kikao hicho, Mbunge wa Segerea, Mhe. Agnesta Kaiza amesema DAWASA inapaswa kuboresha utendaji kazi pamoja na kutatua changamoto kwa weledi na ufanisi ili kuchochea upatikanaji bora wa maji utakaoridhisha wananchi.

"Wananchi wetu wanastahili kupata huduma ya maji bila usumbufu, changamoto tulizozipokea leo ni muhimu sana, na naamini kwa ushirikiano wa karibu kati yetu na DAWASA.

Tutaharakisha utekelezaji wa maboresho katika maeneo yote yaliyobainishwa. Nimejipanga kufuatilia hatua kwa hatua hadi pale huduma zitakapopatikana katika ubora unaotakiwa," amesema Mhe. Agnesta.

Kwa upande wake, Afisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Mhandisi Mkama Bwire amesisitiza dhamira ya Mamlaka ni kuboresha huduma kwa wananchi ili kukidhi matakwa ya Wananchi na kuchochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

"Tumechukua kila changamoto iliyoletwa mezani kwa uzito wake. DAWASA tunakwenda kuongeza nguvu katika mtandao wa usambazaji maji ambapo tutatenga siku maalum za kuleta maji na kufuatilia katika maeneo yote korofi.

Pia tutafanya ukarabati kwenye miundombinu iliyochakaa na kuhakikisha maeneo yote ya Segerea yanapata maji ya uhakika. Ushirikiano wetu na Mbunge utarahisisha utekelezaji wa kazi hizi," amesema Afisa Mtendaji Mkuu.





# Matumaini mapya Nzasa, Somelo na Zingiziwa kupata Maji

Wakazi wa maeneo ya Nzasa, Somelo na Zingiziwa, Wilaya ya Ilala wameanza kuona nuru ya matumaini ya upatikanji wa maji baada kisima kipya cha maji kinachochimbwa ofisi ya kata Zingiziwa kufikia hatua ya asilimia 95.

Kisima hicho kinatarajiwa kuzalisha takribani lita milioni 3.6 za maji kwa siku, hatua inayotajwa ni mkombozi kwa wakazi wa maeneo hayo waliokuwa wanakabiliwa na uhaba wa maji kwa muda mrefu.

Uchimbaji wa kisima hicho ni sehemu ya utekelezaji wa mradi wa maji Nzasa - Somelo unaotekelezwa kwa ushirikiano kati ya Benki ya Dunia (WB) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa gharama ya takribani shilingi bilioni 12.

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) ndiyo imepewa jukumu la kutekeleza ukihusisha ujenzi wa tenki la lita milioni 2, ulazaji wa mabomba kwa umbali wa kilomita 75.

Mhandisi Aziz Namanga, msimamizi wa miradi ya maji pembezoni amesema kazi ya uchimbaji wa kisima imefikia asilimia 95 ambapo tayari majaribio mbalimbali ikiwemo kupima uwingi wa maji yamefanyika.

“Kazi inaendelea ambapo tunatarajia kukamilisha kazi ya uchimbaji, ulazaji wa bomba kuelekea kwenye tenki pamoja na mfumo wa kusukuma maji mwezi Desemba, tumejiridhisha kisima hiki kina uwezo wa kuhudumia maeneo haya hivyo tuwaombe wananchi subira wakati tukiendelea na kazi hii,» amesema.

Afisa Mtendaji wa Kata ya Zingiziwa, ndugu Erick Ishengoma amesema hali ya maji katika mitaa ya kata hiyo haina huduma ya maji ya kuridhisha hali inayowalazimu wananchi kutegemea visima vifupi ili kupata maji kwa ajili ya mahitaji yao ya kila siku.

“Tunashukuru kwa juhudi hizi za Serikali za kuhakikisha hata sisi tulio pembezoni tunanufaika na maji safi na salama, niwapongeze DAWASA kwa ushirikishwaji na juhudi zao za wazi za kutafuta suluhu ya Maji katika eneo letu,» amesema ndugu Ishengoma.

Ndugu Leila Kipuga, mkazi wa mtaa wa Ngobedi, Zingiziwa amepongeza hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi huo kwani unakwenda kumaliza changamoto ya upatikanaji wa maji ikiwemo kufuata maji umbali mrefu nyakati za asubuhi.

«Tulipoambiwa kuhusu utekelezaji wa mradi huu kwa kweli tulijawa na furaha na matumaini kwani nasi tunakwenda kupata maji masafi katika makazi yetu, niwaombe DAWASA kukamilisha kazi hii haraka ili nasi tunufaike,» amesema.

Mradi wa maji Nzasa - Somelo ni moja ya miradi ya kimkakati inayotekelezwa na DAWASA kwa lengo la kuondoa changamoto ya maji kwa wananchi walio pembezoni mwa mji na kuboresha hali ya maisha.

# DC Msando aridhishwa uzalishaji Maji Ruvu Juu, atoa maagizo DAWASA

Mkuu wa Wilaya ya Ubungo (DC), Mheshimiwa Albert Msando amefanya ziara katika mtambo wa uzalishaji maji Ruvu Juu kwa lengo la kuona na kujiridhisha hali ya uzalishaji wa maji katika mtambo huo ambao unahudumia sehemu kubwa ya Wilaya ya Ubungo.

Katika ziara yake hiyo aliyoambatana na Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilaya ya Ubungo pamoja na watendaji wa DAWASA, DC Msando ameridhishwa na hali ya uzalishaji maji huku akitoa maagizo kwa DAWASA kutatua changamoto zilizopo kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji.

"Tumefika hapa Ruvu Juu na tumejiridhisha uzalishaji wa maji upo vizuri, tunafahamu kulikuwa na matengenezo yanaendelea na kusababisha baadhi ya maeneo kukosa maji tumeona matengenezo yamekamilika na huduma inarejea kwa wananchi," amesema Msando

Msando ametoa maagizo kwa watendaji wa DAWASA hasa waliopo Wilaya ya Ubungo kuhakikisha maji yanayozalishwa yanawafikia wananchi bila kikwazo na kutoa taarifa kwa wakati pale panapotokea changamoto yeyote ya huduma lakini zaidi wanaopata maji kwa migao wajue siku gani wanapata na ratiba hiyo isimamiwe bila kupindishwa.

"Nirudie kusema tena, swala la upotevu wa maji halikubaliki, Serikali inatumia gharama kubwa kuchakata maji haya mpaka yanapomfikia mteja uwekezaji huu lazima uthaminiwe na tusimamie vyema kila mwananchi apate maji," amesema Msando.

Meneja wa Mtambo wa uzalishaji maji Ruvu Juu, Mhandisi Juma Kasekwa amesema kwasasa hali ya uzalishaji imerejea katika hali ya kawaida na maeneo yaliyokuwa hayapati maji, huduma inaendelea kuimarika.

"Katika hali ya kuboresha uzalishaji maji katika mtambo wetu wa Ruvu Juu, Serikali imetupatia zaidi ya Shilingi bilioni 1 kununua pampu mbili mpya ambazo ni mategemeo yetu mpaka ifikapo mwezi Novemba tutakua tumezifunga na Kuongeza uzalishaji wa maji," amesema Kasekwa.



# DAWASA, wadau wajifungia kujadili usafi wa mazingira

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), imewakutanisha wadau mbalimbali wa sekta ya usafi wa mazingira kujadiliana kwa pamoja jinsi ya kuhamasisha uboreshaji wa usafi wa mazingira katika Jiji la Dar es Salaam na maeneo yaliyo nje ya mtandao.

Akifungua mafunzo hayo, Msimamizi wa miradi wa DAWASA, Mhandisi Fredrick Mujungu amesema mafunzo haya ni sehemu ya jitihada za mamlaka kuimarisha usafi wa mazingira kupitia ushirikiano wa karibu na wadau muhimu huku elimu kwa umma ikiwa ni nguzo kuu ya mafanikio.

"Lengo kuu la mkutano huu ni kutoa elimu ya kutosha kuhusu umuhimu wa kudumisha usafi wa mazingira, matumizi sahihi ya miundombinu ya maji na majitaka, pamoja na kujadili changamoto zinazokwamisha juhudi za pamoja katika sekta hii muhimu," amesema Mhandisi Mujungu.

Kwa upande wake, Mwakilishi kutoka kampuni ya kishauri ya Economic Business Foundation Sanitation Marketing Consultant (EBF), Leonard Sibomana amesema mafunzo haya yataimarisha ushirikiano wa karibu na wadau muhimu pamoja na kuimarisha mahusiano na watoa huduma binafsi katika kuboresha huduma za usafi wa mazingira.

"Changamoto za usafi wa mazingira haziwezi kutatuliwa na mamlaka peke yake. Tunahitaji mshikamano wa pamoja kati ya sekta binafsi, jamii na taasisi mbalimbali ili kuhakikisha maeneo yetu



yanakuwa safi, salama na yenye mazingira rafiki kwa afya ya binadamu," amesema Sibomana.

Naye Katibu wa watoa huduma binafsi wa usafi wa mazingira, Hamis Juma ameipongeza DAWASA kwa kuchukua hatua hiyo ya kuwaleta pamoja na kutoa elimu na kusisitiza mafunzo ya aina hiyo yanapaswa kuwa endelevu na kushirikisha makundi mbalimbali ya kijamii, hususan vijana na wanawake.

Katika mafunzo haya, mada mbalimbali ziliwasilishwa na wataalamu wa afya na mazingira, wakisisitiza umuhimu wa matumizi salama ya vyoo, uondoshaji wa taka ngumu na majitaka, pamoja na athari za uchafuzi wa mazingira kwa afya ya jamii.



# Watumishi wafundwa Uongozi na Maadili

Watumishi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) katika siku ya pili ya semina ya mafunzo ya kujiepusha na rushwa mahala pakazi yanayoendelea ambapo wameaswa kuzingatia uadilifu na kufanya kazi kwa kuzingatia taratibu za utendaji ili kuleta tija na kuboresha huduma kwa Wananchi.



Mkurugenzi wa Huduma kwa Wateja DAWASA CPA Rithamary Lwabulinda amesema kuwa watumishi wanaohusika na kazi ya usomaji wa mita ni nguzo muhimu kwa Taasisi kwa kuwa ndiyo wanaohusiana na wateja moja kwa moja katika kazi zao.

"Nyie ni kundi muhimu sana na lenye kutegemewa na Taasisi, hivyo mnapaswa kuzingatia nidhamu katika kuwahudumia wateja kwa kulinda hadhi ya Taasisi, na wateja waridhike na huduma," amesema Bi Rithamary.

Amesisitiza kuwa utoaji wa huduma kwa wateja pia uzingatie utaratibu uliopo ikiwemo usitishwaji wa huduma kwa wateja baada ya siku 30 za ulipaji wa bili kwa mteja ambaye hatalipa kwa wakati, pia kuwasisitiza wateja kulipa bili zao za maji kwa wakati ili kutimiza malengo yaliyowekwa na Taasisi katika mwaka huu wa fedha.

Mbali na hapo, Bi Rithamary amewaasa wasoma mita kutokujihusisha na vitendo viovu vya wizi wa miundombinu ya maji pamoja na kuwarubuni wateja kwa lengo la kujipatia fedha zisizo za halali, kwa kufanya hivyo ni kosa kisheria.

Kwa upande wake Afisa Mchunguzi kutoka Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa Nchini (PCCB) Bi Janeth Bernard Kafuko amewaeleza Watumishi kuwa ni kosa la jinai kwa Mtumishi wa Umma kujihusisha na vitendo vya udanganyifu ili kupata rushwa.

"Kila mmoja anatakiwa uzingatie kufanya majukumu yake aliyopewa na kiongozi wake na sio nje ya hapo, kwa kuwa kufanya kazi nje ya utaratibu ndiko kunakosababisha kuwepo kwa vitendo vya rushwa," amesema Bi Janeth.

Ameongeza kuwa ufuatiliaji wa malipo ya ankara kwa wateja unatakiwa kuzingatia uadilifu na kujiepusha na rushwa katika fedha za bili za wananchi.

"Watumishi mnatakiwa kuzingatia nidhamu ya hali ya juu na kujiepusha na makosa yanayoweza kuichafua Taasisi na kukuharibia nafasi yako ya kazi, bali mnatakiwa kuiletea sifa njema Taasisi na Serikali kwa ujumla," amesema Bi Janeth.

Calvin James Mtumishi wa DAWASA Kawe ameishukuru DAWASA kwa kuandaa warsha hii ambayo imewapa ujuzi wa kutosha katika utendaji wao wa kazi na kuwapa tahadhari ya kujiepusha na vitendo vya rushwa.

"Semina hii imetusaidia sana kujua namna bora ya utendaji kazi zetu na imetupa kujua sheria na taratibu zilizopo katika utumishi wa Umma," amesema.

Ameshauri Mamlaka iendelee na utaratibu wa kuandaa semina za namna hii ili kutoa ujuzi wa mara kwa mara kwa Watumishi.



*"Watumishi mnatakiwa kuzingatia nidhamu ya hali ya juu na kujiepusha na makosa yanayoweza kuichafua Taasisi na kukuharibia nafasi yako ya kazi, bali mnatakiwa kuiletea sifa njema Taasisi na Serikali kwa ujumla," amesema Bi Janeth.*

# Miundombinu ya Majitaka Kariakoo kusafishwa saa 24

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), imeweka kambi maalumu ya saa 24 katika eneo la Kariakoo ya kuikarabati miundombinu ya usafirishaji na utiririshaji majitaka ili kuyaweka mazingira kwenye hali ya usafi na salama.


Akizungumzia utekelezaji wa kazi hiyo, Msimaizi wa miundombinu ya majitaka wa DAWASA, Mhandisi Mbaraka Mpala amesema kazi hii ni moja ya kipaumbele cha Mamlaka katika kuboresha usafi wa mazingira eneo la Kariakoo na kufanya biashara zifanyike katika hali shwari na yenye usafi.

«Kazi hii tunaifanya usiku zaidi, kwakuwa mazingira ya eneo hili la kibiashara ni ngumu kusafisha wakati wa mchana ambapo watu ni wengi na msongamano ni mkubwa," amesema Mhandisi Mpala na kuongeza:

"Tunasafisha miundombinu hii ili tumalize tatizo la kuziba mara kwa mara na kutiririsha majitaka mtaani jambo ambalo linahatarisha afya ya wafanyabiashara na wanunuzi wanaoingia na kutoka hapa hali inayosababishwa zaidi na utupaji wa taka ngumu katika mifumo ya majitaka kama vile nguo, mawe, matairi na plastiki.»

Mmoja wa wafanyabiashara katika soko la Kariakoo, Lameck Nganjiro amepongeza utaratibu huu wa DAWASA kusafisha miundombinu hii ya majitaka hususani wakati wa usiku ambapo msongamano na shughuli za kibiashara unakuwa umepungua.

«Kariakoo ni eneo linalopokea watu wengi kwa siku, matumizi ya maji yanayogeuka kuwa majitaka ni makubwa sana, miundombinu hii isipoangaliwa mara kwa mara itatumika isivyo sawa na kusababisha kadhia katika eneo hili majitaka yatakapotiririka mitaani, juhudi hizi za DAWASA ni jambo kubwa na tunawapongeza kwa hatua hii,» amesema Lameck.





*Mafundi wakiendelea na kazi ya uboreshaji wa mitambo ya kuzalisha maji.*



*Mafundi wakiendelea na kazi ya uboreshaji wa mitambo ya kuzalisha maji.*



*Muonekano wa ujenzi wa Bwawa la Kidunda ambao kwa sasa umefikia asilimia 40.*



*Muonekano wa ujenzi wa Bwawa la Kidunda ambao kwa sasa umefikia asilimia 40.*



*Muonekano wa ujenzi wa Bwawa la Kidunda ambao kwa sasa umefikia asilimia 40.*

# Matukio katika picha



*Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) ilikabidhi mchango wa Shilingi Milioni 5 na mifuko 100 ya saruji kwa Shule ya Msingi Msumi Wilayani Ubungo ili kukamilisha ujenzi wa madarasa matatu.*

*Mchango huo ni ahadi aliyoitoa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Aweso wakati akizungumza na wananchi katika mkutano wa hadhara mtaa wa Msumi.*



*Afisa wa DAWASA wakimuonesha mteja usomaji mita shirikishi*



*Maafisa wa DAWASA wakimuonesha mteja usomaji mita shirikishi*



*Kazi za Usafi wa Mazingira usiku na mchana kuliweka Jiji katika hali ya usafi*



*Wanafunzi wa Shule ya Msingi Msumi Wilayani Ubungo wakiwa wameshika mfano wa hundi ya Shilingi Milioni 5 iliyotolewa na DAWASA.*

# Milioni 237 kuboresha Huduma Kinzudi





Wakazi zaidi ya 500 wa mtaa wa Kinzudi, Kata ya Goba, Wilaya ya Ubungo wataanza kunufaika na maboresho ya huduma ya majisafi yanayonywa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es es Salaam (DAWASA).

Maboresho haya yanafanyika baada ya uhitaji mkubwa wa huduma ya maji katika eneo hilo ambalo lilikuwa likipata huduma ya maji kwa msukumo mdogo.

Akizungumzia maboresho yaliyofanyika, Mhandisi Jelson Charles amesema kazi hii upo mbioni kukamilika na ifikapo mwishoni mwa Agosti 2025 wananchi wa mtaa wa Kinzudi watasahau changamoto ya uhaba wa maji.

«Baada ya kupokea taarifa, upungufu wa huduma katika mtaa huu, Mamlaka ilijiridhisha na kuja na mradi wa kuboresha msukumo wa maji ambao umehusisha uchimbaji na ulazaji wa bomba za ukubwa wa inchi 8, 6, na 4 kwa umbali wa Kilomita 3.5, kazi ambayo hadi leo imefikia asilimia 95,» amesema Mhandisi Jelson.

Jelson amesema mradi huu unaogharimu kiasi cha Shilingi Milioni 237, utanufaisha zaidi ya wakazi 500 kwa kuwapatia huduma ya majisafi, salama na toshelevu kwa wakati wote huku akiwaondoa hofu wakazi wa Kinzudi kuwa hakuna ataerukwa katika kupatiwa huduma ya majisafi.

Kwa upande wake, Ndugu Iddy Nyamlani, mkazi wa mtaa wa Kinzudi ameipongeza DAWASA kwa kusikia na kutatua changamoto hii ya upungufu wa huduma katika mtaa wao na sasa wanaimami kubwa ya kuwa na huduma bora wakati wote.

«Tulikuwa hatuna uhakika wa huduma ya maji, yalikuwa yakitoka mara moja moja na hujui ni muda gani yatakatika, lakini kwa kazi hii kubwa tunayoishuhudia ambayo DAWASA wapo mbioni kuikamilisha, tunapata matumaini ya kuwa na huduma bora na endelevu ya maji wakati wote,» ameeleza Ndugu Nyamlani.



# Hoja za Wananchi Matosa zapatiwa ufumbuzi

Wakazi takribani 491 wa maeneo ya Kings, Ruaha na Kwa Msami katika Kata ya Kimara wilayani Ubungo, wanatarajia kupata afueni ya kudumu ya huduma ya maji baada ya kutambulishwa rasmi kwa mradi mdogo wa upanuzi wa mtandao wa maji wa Matosa ulioanza kutekelezwa.

Mradi huo, unaotekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), unalenga kuboresha huduma ya maji kwa kaya takribani 800 maeneo ya Goba, Mbezi na Matosa, hatua inayotarajiwa kumaliza adha ya kusuasua kwa huduma kwa wakazi wa maeneo hayo.

Mamlaka inatekeleza mradi huu kama sehemu ya mkakati wa kuhakikisha kila mkazi wa Dar es Salaam na Pwani anapata huduma ya maji safi na salama ifikapo mwaka 2030, huku wakisisitiza umuhimu wa ushirikiano wa jamii katika utekelezaji wake.

Akizungumza kuhusu mradi huo, Mhandisi wa Miradi, Ndugu Shija Mbonje amesema mradi unatekelezwa kwa umbali wa Kilomita 13, ikiwa kilomita 1.5 zitatekelezwa eneo la Kings ili kutatua adha ya msukumo mdogo wa maji na mara nyingine ukosefu wa maji eneo hilo.

“Mradi huu unakwenda kujibu hoja za wananchi za muda mrefu, vilevile Mamlaka imejipanga kukamilisha mradi huo kwa wakati ili kuboresha huduma kwa wakazi hao,” amesema Mhandisi Shija.

Naye Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Kilungule B, Ndugu Henry Dimoso akizungumza katika kikao cha utambulisho wa mradi huo amesema utekelezaji wa mradi huo ni habari njema kwa wananchi wake na unatoa matumaini mapya.

“Tunaupokea mradi huu kwa moyo wa shukrani na matumaini makubwa. Tunajua utaleta afueni kwa wakazi wetu na kupunguza adha ya ukosefu wa maji kwa muda mrefu,” amesema Ndugu Dimoso.



# DAWASA yazidi kuchagiza malengo ya Serikali huduma za Maji

Katika hatua ya kufanikisha adhma ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha kila mwananchi anapata huduma ya majisafi kikamilifu, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA)kupitia Mkoa wa kihuduma Mapinga imefanikisha zoezi la utoaji wa vifaa vya maunganisho mapya ya maji kwa wateja 120.

Wananchi wa maeneo ya Kiharaka, Kibosha, Vikawe, Kerege, Kiembeni, Udindivu, Mingoi, Mpiji na Changuhela wamepatiwa vifaa na kufungiwa huduma.

Zoezi hilo limesimamiwa na Mhandisi Hamad Omary, ambapo lilienda sambamba na utoaji wa elimu kwa wananchi juu ya mifumo sahihi ya malipo ya huduma, ulinzi wa miundombinu ya maji pamoja na Mawasiliano rasmi ya Mamlaka kwa Wateja.

Mbali na hapo, Mhandisi Omary aliwakumbusha wananchi kutumia ofisi za DAWASA kupata ufumbuzi wa changamoto zao na kutumia namba ya huduma kwa wateja Mapinga ambayo ni 0734 451863 kwa ajili ya kupata ufumbuzi wa changamoto za kihuduma.



# DAWASA yaukata upepo CRDB Marathon

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) wameungana na taasisi za umma, mashirika binafsi pamoja na wananchi mbalimbali katika mbio za CRDB Marathon zilizofanyika leo Jumapili, Agosti 17, 2025 jijini Dar es Salaam.

Lengo mbio hizo ambazo mgeni rasmi alikuwa Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Mabunge Duniani (IPU) ni kukusanya fedha kusaidia watoto wenye matatizo ya moyo, yatima na familia zisizojiweza.

Akizungumzia kwaniaba ya washiriki wote kutoka DAWASA, Mkuu wa Kitengo cha Mazingira, Mhandisi Modesta Mushi amesema umuhimu wa kushiriki mbio hizo huku akielezea umuhimu wa mazoezi kwa watumishi wote.

«Kwanza nichukue fursa kumshukuru Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu, Mhandisi Mkama Bwire kwa kuruhusu kushiriki katika mbio hizi muhimu.

Kama taasisi tunayohudumia wananchi imekuwa vyema kuungana na wenzetu katika kutimiza lengo la kusaidia jamii yenye uhitaji kwa kuchangia matibabu ya moyo, yatima pamoja na familia zisizojiweza kupitia mbio hizi,» amesema Mhandisi Mushi

Mhandisi Modesta  Mushi amesema uwepo wa DAWASA kushiriki mbio hizi za CRDB Marathon ni chachu kwa watumishi wote kuendelea kupenda mazoezi binafsi na kuimarisha afya zao ili kuupa mwili utayari wa kuhudumia wananchi wakati wowote.

Mbio za CRDB International Marathon kwa mwaka 2025 zimebeba kauli mbiu isemayo «Kasi isambazayo Tabasamu.»






# DAWASA, KASHWASA wabadilishana uzoefu Huduma za Maji

Timu ya uzalishaji na usambazaji maji ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), imetembelea Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama Shinyanga (KASHWASA), kwa ajili ya kubadilishana uzoefu katika sekta ya uzalishaji na usambazaji maji.

Ziara hiyo ya mafunzo imehusisha mafunzo ya kiufundi na ukaguzi katika mtambo wa uzalishaji maji wa Ihelele unaohudumia wakazi wa mikoa sita Mwanza, Shinyanga, Singida, Geita, Tabora na Simiyu.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo, Kiongozi wa timu ya DAWASA, Mkurugenzi wa uzalishaji na usambazaji maji, Mhandisi Leonard Msenyele amebainisha ziara hiyo imekuwa chachu ya kujifunza mbinu mpya za kiufundi zitakazosaidia kuboresha huduma katika Jiji la Dar es Salaam na maeneo jirani.

"Kila ziara kama hii hutupa nafasi ya kuimarisha maarifa na kuongeza ubunifu ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora ya majisafi na salama kwa wakati," amesema Mhandisi Msenyele.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa KASHWASA, Mhandisi Patrick Nzamba akizungumza wakati wa mapokezi ameipongeza DAWASA kwa jitihada za kutaka kujifunza na kuchukua uzoefu kutoka kwa wengine lakini pia kuhimiza ushirikiano wa taasisi.

"Tunaamini kushirikiana na kubadilishana uzoefu na taasisi nyingine za maji nchini ni hatua muhimu ya kuongeza ufanisi na kuimarisha huduma kwa wananchi," amesema Mhandisi Nzamba.

Ziara za mafunzo ni sehemu ya mikakati ya DAWASA katika kuboresha huduma za maji kupitia ushirikiano wa kitaasisi na kujenga uwezo endelevu wa kiutendaji.







# Siku tano za kusaka ujuzi Arusha

> AUWSA tumefurahi kuwapokea wenzetu kutoka DAWASA. Tumewaonesha jinsi tunavyosimamia miradi ya visima kwa kutumia teknolojia na mifumo ya ufuatiliaji ili kuhakikisha wananchi wa Arusha... amesema Ndugu Shushu.

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), imefunga safari kwenda Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Jiji la Arusha (AUWSA) kujifunza uzoefu wa uzalishaji na usambazaji maji hususan kupitia visima virefu pamoja na uendeshaji wake.

Watumishi wa DAWASA kutoka Idara ya Visima na Usambazaji Maji watakuwa huko kwa siku tano ambapo wamepokelewa na Menejimenti ya AUWSA na kisha kupata maelezo ya kitaalamu juu ya jinsi Arusha inavyotegemea na kuendesha miradi ya visima virefu kama chanzo kikuu cha maji kwa wananchi.

Akizungumza wakati wa siku ya kwanza ya ziara hiyo, Kaimu Meneja wa Visima, Mhandisi Francisca Merere amesema ziara hiyo ni mwanzo wa ushirikiano mpana baina ya DAWASA na AUWSA katika kushirikiana kitaalamu, ili kuhakikisha Watanzania wanapata huduma bora, safi na salama ya maji.

«Tumekuja AUWSA kujifunza kutokana na uzoefu wao mkubwa katika kuendesha miradi ya visima. Dar es Salaam tuna mradi wa Kigamboni unaotegemea maji kupitia visima virefu hivyo tunahitaji mbinu bora zaidi za kuongeza uzalishaji na usimamizi wa miradi ya visima. Tunashukuru kwa ukarimu na ushirikiano kutoka AUWSA,» amesema.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira kutoka AUWSA, Mhandisi Upendo Shushu amesema ziara hiyo ni fursa ya kubadilishana uzoefu kwani wote ni watoa huduma za maji kwa wananchi.

''AUWSA tumefurahi kuwapokea wenzetu kutoka DAWASA. Tumewaonesha jinsi tunavyosimamia miradi ya visima kwa kutumia teknolojia na mifumo ya ufuatiliaji ili kuhakikisha wananchi wa Arusha wanapata huduma ya maji kwa uhakika.

Tunaamini uzoefu tuliobadilishana leo utasaidia kuboresha huduma Dar es Salaam na pia kuongeza mshikamano kati ya mamlaka zetu,» amesema Ndugu Shushu.

Mbali na kujifunza mbinu za kiufundi, ziara hiyo pia imelenga kubadilishana mikakati ya kudhibiti upotevu wa maji, kuhakikisha ubora wa huduma kwa wateja na kulinda vyanzo vya maji ili huduma ibaki endelevu.



# Bangulo yafungua fursa mpya za biashara Kitunda

Mradi wa Usambazaji Maji Dar es Salaam ya Kusini (Bangulo) ambao umetekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), umeleta mabadiliko makubwa kwa wakazi wa Kitunda Relini, kata ya Ktunda, Wilaya ya Ilala.

Kupitia mradi huu, wakazi sasa wanapata maji kwa uhakika, hali inayochochea kasi ya maendeleo ya biashara na kuboresha maisha yao.

Awali, wakazi wa Kitunda walikuwa wakitumia visima vya jumuiya ya watumia maji Kitunda na Makamba ambavyo havikuweza kukidhi mahitaji yao kutokana na uhitaji mkubwa uliosababishwa na ongezeko la watu pamoja na changamoto za usambazaji maji.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Kitunda Relini, Ndugu Sospeter Marwa amesema ujio wa mradi wa maji Bangulo umebadilisha kabisa hali ya uchumi wa wakazi wa eneo hilo na kuwa chachu ya ukuaji wa maendeleo.

“Zamani wananchi waliteseka kutafuta maji, lakini sasa kila kaya inaunganishiwa huduma ya bomba, watu sasa wameanzisha biashara mpya kama kuosha magari, migahawa na saluni. DAWASA kwakweli imetuwezesha kujitegemea kiuchumi,” amesema Ndugu Marwa.

Miongoni mwa wajasiriamali wanaofaidika na mradi ni Ndugu Godfrey Abdi anayemiliki kituo cha kuosha magari ambaye amesema kabla ya maji kufika, alilazimika kununua maji kwa bei kubwa kutoka kwa malori au kutumia maji ya kisima jambo lililopunguza faida.

“Sasa maji yapo karibu, gharama zimepungua sana. Naosha magari, pikipiki pamoja na kufua mazuria. DAWASA imetusaidia sana kuinua kipato chetu,” amesema Ndugu Abdi.

Ndugu Mwanahawa Kombo, mfanyabiashara wa kuuza chakula katika eneo hilo amesema huduma ya majisafi imemrahisishia kufanya biashara kwa usafi na ufanisi zaidi hali ambayo imemuongezea wateja.

“Kabla ya maji ya DAWASA, nilikuwa natumia muda mwingi kutafuta maji. Sasa napata maji kwa bomba, na wateja wangu wameongezeka kwa sababu usafi umeimarika,” amesema.

Kupitia mradi wa Bangulo, DAWASA imefanikiwa kuboresha maisha ya maelfu ya wakazi wa Kitunda Relini kwa kuwapatia huduma endelevu ya majisafi. Huduma hiyo imechangia katika uchumi wa wananchi kwa kufungua milango ya fursa mpya za biashara.

# Bombani, Pugu Mpakani waitwa kuunganishiwa Maji

Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) imewataka wakazi katika Kata za Pugu, Gongolamboto na Pugu Stesheni Wilayani Ilala kujitokeza na kuunganishiwa huduma ya maji baada ya kukamilika kwa mradi wa Usambazaji maji Dar es Salaam ya Kusini (Bangulo) na miradi mingine midogo ya kusogeza mtandao wa huduma majumbani kwa wateja.

Melkiad Lyamuya, Afisa huduma kwa wateja DAWASA - Ukonga ameeleza hayo wakati wa kampeni ya nyumba kwa nyumba kuwafikia wateja kupitia dawati la huduma kwa wateja linalofunguliwa eneo la Mwanapindi, Kata ya Pugu Stesheni.

"Kwasasa kazi ya kusogeza mtandao wa miundombinu ya huduma imekamilika na huduma inapatikana hususan Mtaa wa Bombani kwa Kata ya Pugu, Mitaa ya Pugu Mpakani, Pugu Kichangani na Bangulo kwa Kata ya Pugu Stesheni. Vilevile katika mitaa ya Gongolamboto, Ulongoni pamoja na Mtaa wa Markaz katika Kata ya Ukonga, hivyo tunawahimiza wakazi wa maeneo hayo kujitokeza na kuleta maombi yao ili waunganishiwe huduma.," amesema Ndugu Lyamuya.

Aidha, Ndugu Lyamuya ametumia wasaa huo kuwahimiza Wananchi kulinda miundombinu ya maji katika maeneo yao na kutoa taarifa DAWASA kituo cha huduma kwa wateja kupitia namba 181 wanapoona shughuli zinazoathiri miundombinu ya maji au uvujaji.

Jumla ya wakazi 119 wamejitokeza na kuhudumiwa ambapo 81 wamefika kwenye Dawati la huduma na wengine 38 wametembelewa majumbani kupatiwa elimu na kuongeza uelewa juu ya huduma za DAWASA.







# Wakazi 68,000 Zingiziwa na Chanika kunufaika na huduma ya Maji

Wakazi wa maeneo ya Zingiziwa, Msongola na Chanika, Wilaya ya Ilala wana matumaini ya kuanza kupata huduma ya maji, baada kukamilika kwa zoezi la upimaji wa wingi wa maji katika kisima cha maji kilichochimbwa katika ofisi ya kata ya Zingiziwa.

Kisima hicho kilichopo mtaa wa Ngobedi, kata ya Zingiziwa Wilaya ya Ilala kinatarajiwa kuzalisha takribani lita milioni 4.8 kwa siku, kwa hatua hii inayotajwa ni mkombozi kwa wakazi wa maeneo hayo waliokuwa wanakabiliwa na uhaba wa maji kwa muda mrefu.

Mradi wa maji Nzasa - Somelo ni moja ya miradi ya kimkakati inayotekelezwa na DAWASA kwa lengo la kuondoa changamoto ya maji kwa wananchi walio pembezoni mwa mji na kuboresha hali ya maisha.

Akizungumza baada ya kukamilika kwa zoezi hilo, Msimamizi wa miradi DAWASA, Mhandisi Aziz Namanga amesema kazi ya upimaji wa wingi wa maji imekamilika kwa asilimia 100 ambapo tayari majaribio yamefanyika kwa kisima kuonyesha uwezo wa kuzalisha lita 200,000 kwa saa.



“Kazi imefanyika kwa kufanya majaribio ya kuona uwezo wa upatikanaji wa maji katika kisima hiki chenye urefu wa mita 204 na kimeonyesha uwezo wa kuzalisha maji lita 200,000 kwa muda wa saa moja hivyo kufika lita Milioni 4.8 kwa saa 24,» amesema.

Mhandisi Aziz Namanga amesema kisima hicho kitahudumia wakazi takribani 68,600 wa maeneo yaliyopo katika kata ya Zingizwa, Msongola na Chanika na kazi iliyobaki ni ulazaji wa mabomba kwa umbali wa kilomita 75.

«Jumla ya wakazi 68,600 watanufaika na huduma ya Maji kupitia kisima hiki ambapo wakazi 12,700 kutoka kata ya Zingizwa, wakazi 27,800 katika kata ya Msongola na wakazi 27,700 katika kata ya Chanika watanufaika na huduma ya Maji,» ameongeza.

Afisa Mtendaji wa Kata ya Zingiziwa, Ndugu Erick Ishengoma amesema hali ya upatikanaji wa maji kwa wananchi sio ya kuridhisha kutokana na kutegemea visima vifupi binafsi ili kupata maji.

«Niwapongeze DAWASA kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji, matarajio yetu ni kila mwananchi apate huduma ya majisafi kwa ajili ya matumizi,» amesema ndugu Ishengoma.

Ndugu Yustina Robert, mkazi wa mtaa wa Ngobedi, kata ya Zingiziwa amepongeza hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi huo kwani unakwenda kumaliza changamoto ya upatikanaji ya maji ikiwemo kufuata maji kwa umbali mrefu.



# Bilioni 9 zaimarisha mifumo ya Majitaka Kipawa

Wananchi wa Mtaa wa Kipawa, Wilaya ya Ilala, Dar es Salaam wameipongeza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), kwa kukamilisha utekelezaji wa mradi wa uondoshaji majitaka majumbani uliotekelezwa kwa lengo la kukabiliana na uchafuzi wa Mazingira kwenye makazi ya wananchi.

Msimamizi wa Mradi wa Majitaka, Mhandisi Fredrick Mujungu amesema mradi huu wa uondoshaji majitaka majumbani umetekelezwa na DAWASA na kukamilika Julia, mwaka huu kwa lengo la kuimarisha usafi wa mazingira na kuokoa afya za wananchi wa Kipawa.

Mradi huu ambao umegharimu Shilingi Bilioni 9.022 umetekelezwa katika maeneo ambayo hayafikiki kwa usafiri na maeneo ambayo ardhi ina kiasi kikubwa cha maji (water table).

«Tayari jumla ya Kaya 70 zimeshaunganishwa kwenye mfumo wa mradi huu na wameanza kunufaika, kazi inaendelea ya kuunganisha vyoo vya wananchi kwenye mradi,» amesema Mhandisi Mujungu.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Mjimpya, Ndugu Albert Mgoe amesema wananchi wa mtaa wa Mjimpya wameishukuru Serikali kwa kutatua changamoto ya uchafuzi wa mazingira iliyokuwa kero kubwa hasa wakati wa mvua ambapo majitaka yalikuwa yanatiririkia mitaani na kusababisha hatari ya magonjwa ya mlipuko kwa wananchi.

Amesema jitihada hizi zilizotekelezwa na DAWASA zimeleta nafuu kubwa kwa wakazi wengi ambao walikuwa wakipata shida ya kuita magari ya kuondosha majitaka kutokana na barabara kuwa na shida ya kupitika.

«Wakazi wengi huku wanapata shida ya kuondosha majitaka kutokana na barabara kuwa mbovu kupitika na magari ya majitaka, pia mpangilio holela wa makazi,» amesema Ndugu Mgoe.

Mmoja wa wanufaika wa mradi, Ndugu Riziki Mohammed wa mtaa wa Mjimpya Kipawa amesema ilikuwa tatizo kwa maeneo haya ya uswahilini kupata huduma ya kuondosha majitaka, hali hii ilisababisha uchafuzi wa mazingira kwa maeneo mengi ya wananchi, lakini kwa sasa tunaishukuru DAWASA kwa kutuletea mradi huu.

Amesema mradi huu unatusaidia kuboresha afya zetu kwa kuondokana na harufu mbaya ya mara kwa mara pamoja na kuepukana na hatari za magonjwa ya mlipuko.

Naye Peter Charles, mkazi wa Kipawa ameishukuru DAWASA kwa kushirikiana vyema na Serikali za mitaa mpaka mradi huu umekamilika na umeleta unafuu katika makazi yetu.

# DAWASA yaimarisha usalama wa Huduma za Maji

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), kwa kushirikiana na Wizara ya Maji, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) na Bodi ya Bonde la Maji la Wami/Ruvu, inaendelea na zoezi la utambuzi na ukaguzi wa visima na magari binafsi yanayouza maji Dar es Salaam na Pwani ikiwa ni sehemu ya jitihada za Serikali kulinda afya na usalama wa wananchi.

Zoezi hilo endelevu katika maeneo yote ya Kihuduma, limetekelezwa katika maeneo yenye visima binafsi Boko Basihaya na Kituo cha Kuchota Maji kwa magari (Maboza) cha Mapinga limehusisha ukaguzi wa miundombinu ya maji, visima, magari ya maji, matanki pamoja na upimaji wa usalama wa maji na matibabu pale inapobidi.

Akizungumza katika zoezi hilo, Afisa Ubora wa Maji DAWASA, Ndugu Maliweza Shusha amesema zoezi hili linalenga kulinda na kuhakikisha usalama wa afya za watumiaji maji.

"Zoezi hili linatusaidia kujua ubora wa maji na kuhakiki usafi wa magari yanayobeba maji kwenda kwa wananchi, magari ambayo hayajakidhi viwango tunakubaliana yasafishwe na tunayafanyia matibabu kisha kuyawekea stika maalum ambazo zitamsaidia mteja kujua gari lililomletea maji limekaguliwa na linatoka katika chanzo salama," amesema Maliweza.

Naye Mtaalamu wa Maji chini ya Ardhi kutoka Bodi ya Maji Bonde la Wami Ruvu, Ndugu Omary Hashim amesema ni wajibu wa Bonde kuhakikisha taratibu za uchimbaji na matumizi ya visima zinazingatiwa.

"Tunashiriki zoezi hili la ukaguzi wa visima ili kutoa elimu juu ya taratibu za kumiliki visima, utoaji vibali na kupima ubora wa maji ili kuhakikisha walaji wanapata na kutumia maji yenye ubora na viwango vinavyostahili kwa mujibu wa sheria ili kulinda afya na usalama wa wanufaika wa maji hayo ya visima," amesema Ndugu Hashim.

Kwa upande wake Mhandisi Mwandamizi wa Maji na Usafi wa Mazingira, EWURA, Kanda ya Mashariki I, Ndugu Ngugu David Linda ameelezea umuhimu wa zoezi hilo.

"EWURA tunafuatilia utekelezaji wa maagizo mbalimbali tuliyotoa ikiwa ni pamoja na DAWASA kuhakiki usajiri wa magari yanayotoa huduma ya maji, kupima Ubora wa Maji yanayosambazwa na magari ili kuendelea kulinda afya za walaji wakati huu wa ukame" Amesema Mhandisi Linda.

Zoezi hili maalum linalenga kuhakikisha wananchi wanapata maji salama na yenye ubora kutoka vyanzo vinavyotambulika ili kulinda afya zao hususan katika kipindi cha changamoto ya upatikanaji wa huduma ya maji iliyotokana na kupungua kwa uzalishaji katika Mitambo ya Ruvu Chini na Ruvu Juu.







# Bilioni 2.2 kumaliza changamoto ya Maji Msumi

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), imetenga Shilingi Bilioni 2.2 kutafuta Suluhu ya tatizo la upatikanaji wa huduma ya maji katika mtaa wa Msumi, Kata ya Mbezi, wilayani Ubungo.

Mradi mkubwa na wa kimkakati katika mtaa wa Msumi ulioanza kutekelezwa Aprili mwaka huu, unatarajia kukamilika Januari mwakani huku zaidi ya wakazi 47,000 wa Mitaa ya Msumi A, Msumi B, Msumi C pamoja na Tegeta A watanufaika.

Akizungumzia utekelezaji wa mradi huo, msimamizi wa mradi, Mhandisi Aziz Namanga amesema mradi unaendelea kwa kasi na kuwahakikishia wananchi wa eneo la Msumi huduma ya majisafi na salama pindi mradi utakapokamilika.

«Mradi huu umehusisha uchimbaji na ulazaji wa mabomba ya maji yenye ukubwa wa inchi 6, 4, 2, na 1 kwa jumla ya kilomita 14.9, ambapo hadi sasa, kilomita 11 za mabomba tayari zimekwishalazwa na kazi ya ulazaji bomba imefikia asilimia 76,» amesema Mhandisi Namanga.

Namanga amesema mbali na ulazaji wa mabomba, mradi huu pia unahusisha ujenzi wa tenki la kuhifadhia maji lenye ujazo wa lita 500,000, pamoja na mnara wa tenki hilo wenye urefu wa mita 12, ujenzi wa vituo 12 vya kuchotea maji, ufungaji wa pampu na uwekaji wa transfoma ya umeme ambayo ni muhimu kwa uendeshaji wa mifumo ya kusambaza maji.

Ndugu Mohammed Issa, mkazi wa Msumi ameipongeza DAWASA kwakuja na mradi huu kwani awali walipata changamoto ya huduma ya maji na kusababisha gharama za maisha kuongezeka na kuhatarisha afya zao kwa kutumia maji yasiyo na uhakika wa usalama wake.

''Hapa kwetu tumekuwa na changamoto ya huduma ya maji, gharama za maisha zilipanda sana kwa kununua maji kwa bei ghali, kwa mwezi unaweza tumia hadi Shilingi 200,000 kununua maji tu, lakini pia ni maji ambayo hatuna uhakika na usalama wake jambo ambalo limehatarisha afya zetu,'' amesema Ndugu Issa



# DAWASA yawatembelea Wateja wakubwa, yasisitiza ulipaji bili

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), imetembelea wateja wakubwa kupitia mashirika binafsi na Taasisi za Serikali kwa lengo la kuboresha huduma, kubaini changamoto zao pamoja na kuhimizia ulipaji wa bili za maji kwa wakati.

Wateja waliotembelea ni pamoja Shirika la Nyumba ya Taifa (NHC), Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Mashirika Binafsi ni Ubungo Plaza, Kiwanda cha Bomba za Chuma (TSP), Ubungo Business Centre pamoja na Kiwanda cha NIDA Textile.

Afisa Biashara wa DAWASA Magomeni, Bi. Ruth Museru amesema Mamlaka inaendelea na zoezi maalum ya kupitia nyumba kwa nyumba na pia kuwatembelea wateja wakubwa ili kutoa elimu na kufuatilia wateja wenye madeni ya huduma.

"DAWASA Magomeni tunaendelea na zoezi la kuwatembelea wateja wakubwa ambao ni TBS, Shirika la Nyumba la Taifa, Chuo cha Usafirishaji NIT pamoja na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kwa lengo la kuwaelimisha kuhusu huduma, kuwahamasisha ulipaji wa bili za maji kwa wakati pamoja na kupokea changamoto za huduma," ameeleza.


Aidha, Bi. Museru ametoa rai kuwa lengo la Mamlaka ni kutoa huduma bora inayokidhi matarajio ya wateja na kuhakikisha huduma ilipwe kwa wakati.

> **Nimefurahi DAWASA kutufikia taasisi yetu leo, ni jitihada kubwa lakini bado kuna haja ya kutoa elimu zaidi juu ya ulipaji wa bili za maji ili kuisaidia Mamlaka kuweza kuboresha huduma zake**

"Mara kwa mara tunaendelea kuwakumbusha wateja juu ya ulipaji wa bili za maji kwa wakati ili kupunguza malimbikizo ya madeni ambayo yanaweza kuathiri upatikanaji wa huduma ya maji endapo hayatolipwa kwa wakati na tumefurahi kuona wateja wanaridhika na huduma zetu na kuahidi kuongeza ushirikiano ili kuboresha zaidi," amesema.

Kwa upande wake, Johnson Lema ambaye ni Afisa Fedha kutoka Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), ikiwa ni sehemu ya Taasisi za Serikali zilizotembelewa ameipongeza DAWASA na kutoa wito kuzidi kuboresha zaidi huduma kwa wateja kwa kuongeza wigo kwa wateja kutoa mrejesho wa huduma kwa Mamlaka ili panapohitajika maboresho ya kihuduma yafanyike.

"Nimefurahi DAWASA kutufikia taasisi yetu leo, ni jitihada kubwa lakini bado kuna haja ya kutoa elimu zaidi juu ya ulipaji wa bili za maji ili kuisaidia Mamlaka kuweza kuboresha huduma zake," amesema.



# DAWASA, Exim Benki ya Korea wakutana, wakubaliana kuimarisha Huduma za Maji Dar

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Mamlaka ya Majisafi na Usafiri wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), Mhandisi Romanus Mwang'ingo amekutana na ujumbe kutoka Benki ya Exim ya Korea ili kuzungumza ni kwajinsi gani kwa pamoja wanaweza kushirikiana kutoa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira kwa wananchi.

"Lengo la kukutana kwetu ni kuboresha urafiki uliodumu kwa muda mrefu kati ya DAWASA na Benki ya Exim kutoka Korea, lakini zaidi kuwapitisha katika mipango yetu ili kwa pamoja tuone wapi tunaweza kushirikiana na wananchi wakapata huduma hususani utekelezaji wa miradi mikubwa na yakimkakati," amesema Mhandisi Mwang'ingo.

Mhandisi Mwang'ingo amesema ipo miradi mikubwa na ya kimkakati ambayo ikitekelezwa na kukamilika itasaidia sana wananchi wa Jiji la Dar es Salaam na Mkoa wa Pwani, miradi kama vile kutoa maji Mto Rufiji, Mradi wa Kuongeza uwezo wa kuzalisha maji katika mtambo wa Ruvu chini na mradi wa Usafi wa Mazingira Buguruni, hivyo ni vyema wakakutana na wadau kama hawa kuwashirikishaa mipango na kuona ni kwa namna gani wanaweza kushirikiana.

Kwa upande wake, Mwakilishi Mkuu kutoka Benki ya Exim ya Korea, Ndugu Kim Kyeang - gu amesema Benki ya Exim Korea imeendelea kuwa na utayari kushirikiana na wadau mbalimbali kuboresha huduma za jamii na wataangalia ni wapi wataweza kushirikiana na DAWASA kuboresha huduma.

"Tumepitishwa katika mipango ya DAWASA, tutakaa na kuchambua vyema kuona ni wapi tunaweza tukashirikiana kuboresha huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira kwa wananchi tukitambua huduma ya majisafi ni kipaumbele kwa wananchi," amesema Ndugu Kim.



# DAWASA yaja na mikakati upungufu wa Maji

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amesema kuwa Serikali kwa kushirikiana na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam DAWASA inaendelea na mkakati wa kuhakikisha huduma ya majisafi inaimarika na kupatikana kwa wananchi wote ili kukabiliana na upungufu wa maji.

Amesema kuwa changamoto iliyopo ya maji ni kutokana na kuchelewa kwa mvua za masika zilizotarajiwa kunyesha kwa kipindi cha mwezi wa kumi na mwezi wa kumi na moja.

Mhe. Aweso amekumbushia maagizo mahususi aliyoyatoa kwa Mamlaka ya kuhakikisha kiasi cha maji kilichopo kwa sasa kinagawanywa kwa wananchi kwa usawa kulingana na ratiba ya usambazaji maji inavyoelekeza.

"Wananchi wapate maji ipasavyo kulingana na ratiba ya usambazaji inavyoelekeza ili kila mwananchi apate maji japo kwa saa chache," ameeleza.

Afisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA Mhandisi Mkama Bwire ameeleza sababu zilizosababisha changamoto hii kuwa ni pamoja na kuchelewa kwa mvua za vuli zilizotarajiwa kunyesha katika mwezi wa kumi hadi mwezi wa kumi na mbili.

Pia ni kutokana na Mto Ruvu kuacha njia yake ya mwelekeo wa maji katika maeneo ya Kitomondo na kutengeneza mchepuko unaotawanyisha maji na kupunguza kiasi cha maji Mtoni.

Ameongeza kwa kusema kuwa ongezeko la shughuli za kilimo ni mojawapo ya sababu zilizosababisha kuharibika kwa chanzo cha maji kwa kuathiri mwelekeo wa maji ya Mto Ruvu. Hivyo jitihada kubwa zinahitajika katika kukabiliana na changamoto hii.

Mbali na hapo Mhandisi Bwire amesema Mamlaka imechukua hatua mbalimbali za kuboresha hali hii ikiwemo kufufua visima vilivyopo katika maeneo mbalimbali ya Jiji ili viweze kutumika kama mbadala wa kuongeza upatikanaji wa majisafi kwa wananchi.

"Tunajitahidi kuongeza nguvu kubwa katika kudhibiti upotevu wa maji mitaani ili maji yanayopotea yaweze kuingia kwenye mfumo na kuhudumia wananchi," amesema Mhandisi Bwire.

Naye Mkurugenzi wa Bonde la Maji Wami Ruvu Mhandisi Elibariki Mmasi amebainisha kuwa upungufu wa maji katika Mto Ruvu umesababishwa na mabadiliko ya tabia nchi linalosababisha ongezeko la joto la wastani wa digrii 2.3.

Amesema hatua zilizochukuliwa ikiwa ni pamoja na kusitisha utoaji wa vibali kwa Watumiaji wa skimu za umwagiliaji hususani katika kipindi hiki cha kiangazi.

# Mlandizi waunganishiwa Huduma za Maji

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) imesema, ndani ya mwezi huu wa Septemba, zaidi ya wateja 300 wa Kata za Vigwaza, Janga, Mtongani na Kawawa wataunganishiwa huduma ya maji.

Hatua hiyo ya uunganisha maji unaofanhwa na DAWASA, Mkoa wa Kihuduma Mlandizi ni kuendelea kutimiza malengo ya Serikali ya kuhakikisha wananchi wanapata maji safi na salama kwa zaidi ya asilimia 85.

Akizungumza wakati wa zoezi la ugawaji vifaa vya maunganisho, Mhandisi Ally Migeyo amesema ni sehemu ya mkakati wa Mamlaka kuhakikisha kila mkazi wa Mlandizi anaunganishwa na huduma ya maji safi ili kuboresha afya na ustawi wa jamii katika maeneo mbalimbali hasa yanayoendela kukua kwa kwasi kama Mlandizi.

"Huduma ya maji ni haki ya msingi kwa kila mwananchi na uunganishaji huu, umewekwa kama sehemu ya mkakati wa Mamlaka wa kupanua wigo wa huduma zake pamoja na kuimarisha miundombinu ya upatikanaji wa maji safi kwa jamii bila usumbufu wa kutembea umbali mrefu au kutegemea vyanzo visivyo salama," amesema Meneja huyo.

Mkazi wa Kijiji cha Mnindi, Ndugu Swaum Ramadhan ameishukuru DAWASA kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuhakikisha kila mwananchi anapata huduma ya maji, hii imeleta faraja sana faraja kubwa kwani adha ya kutumia muda mwingi kutafuta maji badala ya kushughulikia shughuli za maendeleo, imekwisha

"Hatua ya kuletewa vifaa vya maunganisho ya huduma katika maeneo yetu, ni faraja sana kwetu, kwani imeokoa muda kwa kupata huduma hii ndani ya muda mfupi kutasaidia hata kuboresha shughuli za kiuchumi, ikiwemo biashara ndogo ndogo zinazohitaji maji ya uhakika," amesema.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa mtaa wa Janga, Ndugu Sharifu Hassan amesema furaha yake kuona DAWASA wamewafuata majumbani kwao ili tu kuhakikisha kwamba kila mwananchi anapata huduma ya maji kwa wakati na kwa muda mfupi.

"Jambo hili la kuwaletea wananchi vifaa vya maunganisho majumbani, na kuhakikisha kila aliyeomba huduma amenufaika ni jambo la baraka sana, tunawashukuru sana na kuwapongeza katika utumishi wenu," amesema Ndugu Hassan.







# DAWASA, Korea waweka mikakati kuboresha Huduma za Maji

Ujumbe wa wabunge kutoka nchini Korea na wawakilishi wa Benki ya Exim Korea wametembelea Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) na kukubaliana kuimarisha ushirikiano wa usimamizi na usambazaji wa huduma za maji.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo, Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Mhandisi Mkama Bwire amesema Tanzania ina vyanzo vingi vya maji lakini changamoto iliyopo ni usimamizi na usambazaji wa rasilimali hii kwa wananchi.



«Nchi yetu haina shida ya maji, tuna vyanzo vingi vya maji kama vile mito na maziwa makubwa mfano Mto Ruvu ambao unachukua asilimia 90 ya maji yanayosambazwa katika Jiji la Dar es Salaam.

"Kupitia ujumbe huu wa nchi ya Korea, tunatarajia zaidi kuendeleza miradi ya uboreshaji huduma za maji na kukabili changamoto ya upotevu wa maji katika maeneo ya kihuduma,» amesema Mhandisi Bwire.

Kwa upande wake, Kiongozi wa Ujumbe huo, Bi. Lee Jae Jung kwa niaba ya Korea ameridhishwa na jitihada zinazofanywa na DAWASA katika usimamizi na usambazaji wa huduma ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma za maji na Serikali ya Korea itaendeleza ushirikiano huu ili kuchochea na kuendelea jitihada hizo.

Ujumbe huo umefanya mazungumzo na Menejimenti ya DAWASA kuhusu fursa za kuboresha miundombinu ya huduma za maji na teknolojia za kisasa zinazoweza kuongeza ufanisi wa huduma kwa wakazi wa Dar es Salaam na Pwani.

Kupitia ziara hii, DAWASA na washirika hao wa kimataifa wameonesha dhamira ya kuendeleza miradi ya huduma za maji, kuboresha upatikanaji endelevu wa huduma za maji kwa wananchi na kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika sekta ya maji.

# Mwanapindi watafutiwa suluhu ya Maji

Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), imeanza kutekeleza mradi wa kuongeza mtandao wa huduma ya majisafi utakaonufaisha wakazi zaidi ya 500 wa eneo la Mtaa wa Bangulo Mwanapindi, Kata ya Pugu Stesheni, Wilaya ya Ilala.

Mradi huu ni sehemu ya matokeo ya utekelezaji wa mradi mkubwa wa Usambazaji maji Dar es Salaam ya Kusini (Bangulo) uliotekelezwa na DAWASA kwa gharama ya Shilingi Bilioni 36.9.

Akizungumza wakati wa zoezi la ulazaji mabomba ya usambazaji maji katika eneo hilo, Msimamizi wa Mradi Mhandisi Adam Makindai kutoka DAWASA Ukonga amesema mradi huo umeanza kutekelezwa na unatarajiwa kuondoa changamoto ya upatikanaji maji katika mtaa huo.

«Kwasasa tunaendelea na hatua ya uchimbaji mitaro ili kulaza mabomba ya kipenyo cha inchi 1.5», inchi 2 na inchi 3 kwa umbali wa kilomita 12.75 ambapo baada ya kukamilika kwa mradi yatahudumia zaidi ya wakazi 500 na kutatua changamoto ya ukosefu wa majisafi katika eneo la Mwanapindi,» amesema Mhandisi Makindai.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Bangulo, Kata ya Pugu Stesheni, ndugu Goodluck Mwele ameishukuru DAWASA kwa mradi huu ambao utasaidia kuboresha upatikanaji wa majisafi na salama pamoja na kuboresha hali ya uchumi.

«Eneo hili limekuwa na hali ngumu ya upatikanaji wa huduma ya majisafi kwa takriban miaka 10 wananchi wanapata maji yasiyo salama kutoka katika Mabwawa au kununua kwa Shilingi 5,000 au zaidi kwa uniti moja lakini mradi huu unaleta matumaini ya kupata majisafi na salama na kwa gharama ya kumudu ambayo ni 1,679.63 kwa unit moja,» amesema ndugu Mwele.

Mkazi wa Mwanapindi, ndugu Anna Joseph Lyimo ameishukuru Serikali ya Mheshimiwa Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwaondolea kero ya maji ambayo imewatesa kwa muda mrefu.

«Kwakweli tunapata shida sana ya maji, ni tabu kuyapata na tunanunua kwa gharama kubwa ambayo sio kila mtu anaimudu, mradi huu utatukomboa akina mama na kupunguza gharama za kununua maji,» amesema ndugu Anna.





# DAWASA yawanoa Viongozi usimamizi bora wa utendaji

Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) imeendesha mafunzo ya uhamasishaji na kuongeza uelewa juu ya usimamizi na upimaji wa viashiria vya utendaji kazi kwa kwa viongozi waandamizi wa Idara na vitengo ili kuongeza ufanisi na kuboresha utendaji kazi kwa watumishi.

Kupitia mafunzo hayo, DAWASA inalenga kuoanisha malengo ya kila mtumishi na malengo ya kimkakati ya taasisi na kufuatilia utekelezaji wa shughuli kwa kutumia viashiria vya utendaji.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa mafunzo hayo, Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Mhandisi Mkama Bwire amesema mpango wa usimamizi na upimaji utendaji wa watumishi utasaidia utekelezaji bora wa mipango na muelekeo wa Mamlaka katika kuhudumia wananchi.

"Watumishi tunapaswa kujikita katika kutekeleza malengo muhimu zaidi na kuhakikisha tunachukua hatua za kimkakati, kiuwajibikaji ili kupata matokeo chanya ya malengo na kuwasilisha taarifa sahihi kwa wakati," amesema Mhandisi Bwire.

Mafunzo haya ya kuwaongezea ufahamu watumishi unajumuisha ukaguzi wa mara kwa mara wa ndani, tathmini za miezi na mwaka pamoja na matumizi ya mifumo mbalimbali ya kidigitali ili kuhakikisha matokeo sahihi yanayotarajiwa yanapatikana kwa wakati.

DAWASA imewahakikishia wananchi itaendelea kutoa huduma bora na za uhakika, huku ikihimiza ushiriki wa wananchi katika kutoa taarifa na mapendekezo ili kuboresha zaidi huduma zinazotolewa.







# DAWASA inavyowafikia Wateja na 'Maji kiganjani'

**"Utaratibu huu utarahisisha uunganishaji wa huduma ya maji kwa wananchi, watumishi wetu wapo mtaani kuhakikisha kila aliefikia vigezo vya kupata huduma anapatiwa vifaa vyake na Kuunganishiwa huduma kwa haraka, hii itatusaidia kuongeza idadi ya wananchi tunaowahudumia," amesema Mhandisi Kavishe.**

Wananchi mbalimbali katika maneno ya Kibamba na Mivumoni wamepongeza utaratibu wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), kuwarahisishia huduma kwa kuwapelekea vifaa vya maunganisho mapya majumbani na kuwaungia huduma kwa wepesi.

Zaidi ya kaya 80 kutoka mitaa ya Mpiji Magohe, Mloganzila, Kiluvya Madukani, Makurunge, Nyakasangwe, Tegeta A na Madale wamefikiwa na kupatiwa vifaa hivyo.

Ndugu Abiud Shayo, mkazi wa Kata ya Kiluvya amesema utaratibu huu unapunguza umbali wa wateja kufata vifaa wenyewe katika ofisini za DAWASA lakini unaharakisha zoezi la kuunganishwa na huduma ya maji kwa kutumia muda mfupi.

"Tunapunguza gharama nyingi kufatilia vifaa wenyewe katika ofisi za DAWASA na kupunguza umbali, muda mwingi sasa tutaendelea na shughuli zetu za kawaida huku tukiwa na uhakika wa kupatiwa vifaa na kuunganishwa na huduma ya maji, kwa hili niwapongeze DAWASA," amesema Ndugu Shayo.

Mhandisi Mkashida Kavishe, Meneja wa Mkoa wa Kihuduma DAWASA Kibamba amesena lengo kubwa la kupeleka vifaa kwa wananchi ni pamoja na kusogeza huduma zaidi na kuharakisha zoezi la maunganisho ya majisafi kwa wateja ambao wameshakamilisha taratibu zote za kupatiwa huduma.

"Utaratibu huu utarahisisha uunganishaji wa huduma ya maji kwa wananchi, watumishi wetu wapo mtaani kuhakikisha kila aliefikia vigezo vya kupata huduma anapatiwa vifaa vyake na Kuunganishiwa huduma kwa haraka, hii itatusaidia kuongeza idadi ya wananchi tunaowahudumia," amesema Mhandisi Kavishe.




# Wiki ya Huduma kwa Wateja yaadhimishwa kwa Wananchi

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), imeendesha dawati la huduma kwa wateja kwa lengo la kuwafikia wateja wengi kwa ukaribu zaidi na kutatua changamoto mbalimbali pamoja na kukusanya maoni juu ya uboreshaji wa huduma ya maji na usafi wa mazingira.

Hatua hii, ni katika kuadhimisha Wiki ya huduma kwa wateja kwa mwaka 2025 iliyobeba kauli mbiu isemayo «Dhamira inayowezekana.»

Akizungumza katika dawati hilo la huduma kwa wateja, Meneja wa Huduma kwa Wateja DAWASA, Ndugu Doreen Kiwango amesema wiki hii ni muhimu sana kwa Taasisi kwani inakumbusha uhusiano uliopo kati ya Mamlaka na wateja wake, hivyo ni muhimu kuwafikia na kuwasikiliza.

«Leo tupo hapa mtaa wa Bangulo Mwembekiboko, kata ya Pugu Station, mteja anapofika hapa tunamsikiliza changamoto na maoni yake, lakini huduma ya kuunganishiwa maji, changamoto za ankara, wateja ambao hawapati maji wote tunawahudumia katika dawati hili,» amesema Kiwango.

Wananchi waliofika katika dawati hilo, wameishukuru DAWASA kwa kuwasogezea huduma karibu hasa katika kipindi hiki cha wiki ya huduma kwa wateja kwani inaonyesha kwa vitendo jinsi gani wanawajali wateja wao.

«Leo tunapata huduma tukiwa hapa mtaani kwetu, tunaipongeza DAWASA hasa tukiadhimisha wiki hii ya huduma kwa wateja, tumetatuliwa changamoto zetu kwa wepesi sana na tunaomba baada ya hapa utaratibu huu uwe wa mara kwa mara,» amesema Ndugu Ally Hassan.

Dawati hili la huduma kwa wateja lilitanguliwa na watumishi wa DAWASA kupita mtaa kwa mtaa kusikiliza wananchi na kutatua changamoto zao pamoja na kupokea maoni juu ya kuboresha huduma ya maji na usafi wa mazingira.

# Mtaa kwa mtaa wiki ya huduma kwa Wateja Kinondoni

Katika kuhitimisha wiki ya huduma kwa wateja inayoadhimishwa Oktoba 6-10 kila mwaka, Mkoa wa kihuduma DAWASA Kinondoni imewatembelea wateja, kusikiliza na kutatua changamoto za kihuduma kwa lengo la kuboresha huduma.

Meneja mkoa wa kihuduma DAWASA Kinondoni, Ndugu Tumaini Muhondwa amesema hizi ni jitihada za Mamlaka za kuwafikia wateja karibu katika kuthamini nafasi yao pamoja na kutoa ushirikiano kwao.



"Tumewatembelea wateja wetu katika eneo letu la kihudum kwa lengo la kuwashukuru wateja kwa kuendelea kutuamini na tunaahidi kuwapa ushirikiano wa kutosha ili huduma ya maji iweze kuwafikia kwa ubora zaidi," amesema Ndugu Muhondwa.

Ndugu Muhondwa amesema katika kuwafikia wateja hao pia walifanikiwa kutoa elimu ya utunzaji wa miundombinu ya maji, ulipaji wa bili za Maji kwa wakati pamoja na kuwapatia elimu juu ya kutoa taarifa na kupunguza upotevu wa maji.

Wateja waliotembelewa ni pamoja na maeneo ya Mwananyamala, Kinondoni, Mikocheni, Msasani, Hananasifu na Kijitonyama. Wateja wakubwa waliotembelewa ni Sea Cliff Hotel, Tanzania Chamber of Commerce Zhe Jiang, Jangid, Airtel, Sheifee Hospital, Shoppers Plaza na US Embassy.

Ndugu Rukia Omary, Mkazi wa Hananasifu ameipongeza DAWASA kwa hatua waliofikia kuwatembelea wateja na kutoa elimu pamoja na kuwathamini nafasi yao na kuahidi kutoa ushirikiano ili kuhakikisha huduma ya maji inazidi kuboreshwa.

Wiki ya huduma kwa wateja mwaka 2025 imebeba kaulimbiu inayosema "Dhamira inayowezekana."





# Mradi wa Maji Salasala - Livingstone kukwamua shughuli za kiuchumi Wazo

Jumla ya wakazi 1,500 watanufaika na maboresho makubwa ya huduma ya maji mtaa wa Salasala kata ya Wazo Wilaya ya Kinondoni.

Ni baada ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kuanza utekelezaji wa mradi wa maji Salasala-Livingstone wenye lengo la kuongeza msukumo wa maji katika eneo hilo.

Mradi wa maji Salasala-Livingstone unaogharimu kiasi cha Shilingi Milioni 203 utahudumia maeneo ya Livingstone, Interchick, Wagiriki, Mbezi tiles, Mapanga Shaa, Luona, Salasala Magengeni , na Nabii Flora kwa kuwapatia huduma bora ya majisafi na endelevu wakati wote.

Akizungumza utekelezaji wa mradi huo, Meneja wa DAWASA mkoa wa kihuduma Tegeta, Mhandisi Edson Robert amesema eneo la Salasala Magengeni na maeneo jirani yalikuwa yakipata maji kwa msukumo mdogo na kusababisha shughuli nyingi za wananchi kukwama jambo ambalo wamelipatia ufumbuzu kupitia mradi huu.

"Mradi huu unahusisha uchimbaji na ulazaji wa bomba lenye ukubwa wa inchi 6 kwa umbali wa kilomita 2.8 na kwa kiasi kikubwa utaimarisha sana huduma sio kwa wateja wa majumbani tu hata wale wakubwa wenye uhitaji wa maji mengi kwa siku huduma itaimarika sana," amesema Mhandisi Edson.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Mtaa wa Salasala, Ndugu Robert Massawe ameipongeza DAWASA kwa usikivu na maamuzi ya haraka kuja na mradi huu ukizingatia wingi wa wakazi katika eneo hili na maeneo ya jirani.

"Eneo letu lina wingi wa wakazi na wanaongezeka kila siku, maji tuliyokuwa tunapata awali hayakukidhi mahitaji yetu, lakini sasa tumepata imani baada ya kuona kasi ya utekelezaji wa mradi huu ambao unakwenda kumaliza kabisa changamoto ya maji hapa mtaani kwetu na maeneo jirani na wananchi kunufaika na shughuli za kiuchumi zinazotegemea huduma ya maji kwa kiasi kikubwa," amesema Massawe.



# Suluhu ya Maji Mbande yapatikana, Wakazi 600 kunufaika

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) inatekeleza mradi mpya wa huduma ya maji kwa wakazi wa Kata ya  Chamanzi, mtaa wa Mbande, Wilaya ya Temeke.

Mradi huo umehusisha ulazaji wa bomba za inchi 6, 4 hadi mbomba la kipenyo cha inchi 2, bomba za inchi 6 imetoka kwenye bomba la kipenyo cha inchi 10.

Mradi una umbali wa kilomita 5.2. Kukamilika kwa mradi huu kutanufaisha wakazi takribani 600  lengo ni kumaliza tatizo la maji kwa wakazi hao.

Akizungumzia mradi huo, Meneja wa DAWASA Mkoa wa Kihuduma Mbagala, Ndugu Julieth John amesema utekelezji wa mradi huo unafanyika kutokana na maeneo hayo kutokuwa na huduma ya maji na kusababisha usumbufu wa upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama.

“Kisewe na Mbande Magengeni ni moja ya maeneo ambayo huduma ya maji ilikuwa haijafika na kupelekea sisi kama DAWASA kutafuta suluhisho la changamoto inayowakabili wananchi wa eneo hili,” amesema Ndugu Julieth

Naye Mhandisi Emmanuel Huja amesema, kutokana na maeneo hayo kuwa na ukosefu wa huduma ya maji  kwa muda mrefu, kumesababisha kuwepo kwa changamoto ya maji ila kwa sasa tatizo hilo linakwenda kumalizika baada ya kazi hii kukamilika.

“Kukamilika kwa kazi hii kutaboresha na kuimarisha huduma ya maji katika maeneo haya maana tunatambua maji ndio kila kitu na sasa adha iliyokuwa mwanzo inakwenda kuisha kwani tuko hatua za mwisho kukamilisha,” amesema Mhandisi Huja.

Kwa upande wa Mwenyekiti wa Mtaa wa Mbande, Ndugu Adam Nikolo  ameishukuru na kuipongeza DAWASA kwa hatua kubwa iliyochukuwa ya  kuondoa changamoto ya maji iliyokuwa imedumu kwa muda mrefu.

“Mimi kama kiongozi wa mtaa huu nakiri tumekuwa na shida ya maji kwa kipindi kirefu na baada ya kupata taarifa ya mradi huu naona tunakwenda kusahau kabisa tatizo hili.

“Nipende kuishukuru DAWASA kwa niaba ya wananchi wangu kwa kutukumbuka na kutusogezea huduma karibu maana tulikuwa tunapata shida sana,” amesema Ndugu Adam Nikole.

Ndugu Ally Juma, mkazi wa Kisewe  ameipongeza DAWASA kwa kuwasogezea huduma ya maji karibu inayokwenda kuondoa  changamoto ya maji iliyowatesa kwa muda mrefu, ameiahidi DAWASA kuwa mjumbe wa kuhamasisha utunzaji wa miundo maji katika eneo lao.

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira DAWASA inafanya kazi kwa bidii kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya majisafi na salama kwa ustawi wa jamii.





# DC Msando mguu kwa mguu Mburahati ufufuaji visima

Mkuu wa Wilaya ya Ubungo (DC), Mheshimiwa Abert Msando ametembelea na kukagua hali ya huduma ya upatikanaji maji kata ya Mburahati wilayani humo huku akitoa maelekezo kufufuliwa kwa visima vinne katika Kata hiyo na wananchi waanze kupata huduma ya maji.

"Leo tumeanza na kata ya Mburahati, tumepita katika visima vinne kwa mama Ndunguru, Kwa Mrosso, CCM na Kwa Simba, visima hivi vina maji ambayo yanaweza kusambazwa kwa wateja na wakapata huduma, vinahitaji marekebesho madogo ambayo naelekeza DAWASA siku ya kesho Jumatatu wakamilishe maboresho hayo na visima viane kufanya kazi," amesema DC Msando.

Msando amesema kata ya Mburahati itakua mfano wa utekelezaji wa maagizo ya Waziri wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Aweso kukufua visima vya akiba ili kusaidia upatikanaji wa maji kwa wananchi katika kipindi hiki cha mpito wa ukame kilochopelekea kupungua ka upatikanaji wa maji kutokana na ukame na mabadiliko ya tambia ya nchi.

"Mimi binafsi pamoja na timu ya wataalamu wa visima DAWASA tutashinda hapa Mburahati siku ya kesho kuhakikisha maagizo niliyotoa yanatekelezwa na hii itathibitisha ushirikiano mzuri kati ya serikali za mitaa, DAWASA pamoja na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya katika kuwahudumia wananchi," amesema DC Msando.

Kwa upande wake, Afisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Mhandisi Makama Bwire amesema maelekezo ya Mkuu wa Wilaya wameyapokea na utekelezaji wake unaanza mara moja hii leo ili ndani ya muda mfupi wananchi hawa waendelee kupata huduma ya maji.

"Lakini pia kama Mkuu wa Wilaya alivyoeleza, tukipata listi ya visima vyote katika mitaa mbalimbali ya Dar es Salaam kutoka kwa wenyeviti na watendaji wa serikali za mitaa vilivyopo katika maeneo yao itasaidia kuvitambua kwa uharaka na kufanya maboresho ili viendelee kusaidia wananchi kuwapatia huduma ya maji," amesema Mhandisi Bwire.

MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA DAR ES SALAAM

# MALIPO YA HUDUMA ZA MAJI DAWASA KUPITIA MITANDAO YA SIMU

Ndugu Mteja, kulipia huduma ya maji kwa njia ya mitandao ya simu ni rahisi sana fuata hatua zifuatazo:

**m-pesa**

Bofya *150*00#
- Chagua 4 (Lipa kwa M-PESA)
- Chagua 5 (Malipo ya Serikali)
- Chagua 1 (Weka kumbukumbu)
- Weka namba ya siri na kamilisha muamala

**Mixx**

Bofya *150*01#
- Chagua 4 (Lipa Bili)
- Chagua 5 (Malipo ya Serikali)
- Weka namba ya Malipo
- Thibitisha Malipo, Lipa yote (1) au lipa kiasi (2)
- Weka namba ya siri na kukamilisha Muamala

**T-PESA**

Bofya *150*71#
- Chagua 4 (Lipa Bili)
- Chagua 5 (Malipo ya Serikali)
- Chagua 1 (Ingiza namba ya Malipo)
- Weka namba ya malipo
- Ingiza kiasi
- Weka namba ya siri kuthibitisha muamala

**airtel**

Bofya *150*60#
- Chagua 5 (Lipa Bili)
- Chagua 5 (Malipo ya Serikali)
- Chagua 1 (Ingiza namba ya Malipo)
- Weka namba ya malipo
- Ingiza kiasi

**halopesa**

Bofya *150*88#
- Chagua 5 (Lipa Bili)
- Chagua 7 (Malipo ya Serikali)
- Chagua 1 (Ingiza namba ya malipo)
- Weka namba ya malipo
- Ingiza kiasi
- Weka namba ya siri kuthibitisha muamala

**LIPA BILI YAKO KWA WAKATI!**

181 Bila Malipo | +255 735 202 121 | dawasatz | www.dawasa.go.tz

# Maili Moja na Mkuza wapatiwa suluhu ya Majisafi

Takribani wateja 350 kutoka katika Kata za Mailimoja, Mkuza, Msangani, Kongowe na Picha ya Ndege, Mkoa wa Pwani, Kibaha wataondokana na changamoto ya upatikanaji wa huduma ya majisafi majumbani mwao baada ya kupokea vifaa na kuungwa rasmi na huduma hiyo.

Zoezi hili linatekelezwa katika Mkoa wa kihuduma Kibaha, ambapo jumla ya wateja 350 wanakwenda kunufaika na huduma hii ndani ya mwezi Novemba.



Akizungumza wakati wa zoezi la ugawaji wa vifaa vya maunganisho ya maji, Mhandisi wa Miradi, Ndugu Emmanuel Charles amesema jumla ya wateja 350 wamepatiwa vifaa, na zoezi la kuwaunganisha na huduma linaendelea, huku akisisitiza zoezi hilo ni endelevu kwa wateja wote walioomba na kukamilisha maombi ya huduma ya maji.

"Wateja hawa 350 tuliowatoa leo ni sehemu ya zoezi endelevu la kuwaungia wananchi huduma ya majisafi, natoa wito kwa wananchi ambao hawana huduma bado kufanya maombi ya huduma ya maji na kulipia huduma hiyo ili tuweze kumuunga na maji kwa haraka. Na kwa wale ambao wameshatuma maombi waweze kulipia ili kupatiwa huduma," amesema Mhandisi Emmauel.

Kwa upande wake, Ndugu Razia Hashim, Mkazi wa Kata ya Picha ya Ndege ameshukuru jitihada zinazofanywa na Mamlaka za kuhakikisha kila mwananchi anapata huduma ya maji kwa wakati.

"Huduma kwa sasa inaridhisha, unapoomba huduma ya maji hukai tena muda mrefu kabla ya kuungiwa maji, tunawashukuru sana kwa kuturahisishia kazi na kuokoa muda wa kufanya shughuli nyingine za nyumbani na za kiuchumi," amesema Ndugu Razia.

Zoezi la maunganisho mapya ya majisafi ni mojawapo ya mkakati wa Serikali wa kuhakikisha huduma ya maji inafika kwa kila mwananchi.







# Milioni 700 kutatua changamoto ya Majitaka Sinza C

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) imeanza utekelezaji wa mradi wa uboreshaji Usafi wa Mazingira mtaa wa Sinza C, Kata ya Sinza Wilaya ya Ubungo, wenye lengo la kutatua changamoto ya utiririshaji majitaka kiholela hali inayohatarisha afya za wananchi.

Kukamilika kwa mradi huu kutanufaisha wakazi wa mitaa ya Mahakama ya Mwanzo, Sinza, Shebofu, Nyamuyo, Msafiri, Sembule, Shirika, mtaa wa Mwanza pamoja na Maneti.

Msimamizi wa mradi kutoka DAWASA, Mhandisi Justine Kyando amesema mradi huu unahusisha uchimbaji na ulazaji wa bomba zenye ukubwa wa inchi 10 kwa umbali wa kilomita 1.5 pamoja na bomba la inchi 8 kwa umbali wa kilomita 2.9 na utakapokamilika utaenda kunufaika kaya takribani 250.

"Mradi huu tumeuanza Novemba 2025, na tunatarajia kukamilisha ifikapo Aprili 2026, mradi unagharimu kiasi cha Shilingi Milioni 700 na kukamilika kwake kutamaliza tatizo la kujaa mara kwa mara kwa chemba za majumbani kunakosababishwa na water table kuwa juu," amesema Mhandisi Kyando.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa mtaa wa Sinza C, Ndugu Fredrick Kapufu ameishukuru Serikali kupitia DAWASA kwakusikiliza ombi lao la kuwekewa mfumo rasmi wa majitaka katika mtaa wao jambo ambalo wananchi wamelipokea vyema.

"Mradi huu umekuja katika wakati sahihi, wananchi wamehamasika sana kujiunga na mfumo wa uondoshaji majitaka ukizingatia wengi wao wamekuwa wakipata huduma kupitia magari ya watoa huduma binafsi ambayo ni gharama kubwa sana, hii itawaletea unafuu wa maisha pamoja kuboresha Mazingira kwa ujumla," amesema Ndugu Kapufu.

Ndugu Jovin Nassoro, Mkazi wa mtaa wa Sinza C ameasa wananchi wenye tabia ya kutiririsha majitaka kiholela mtaani na kuchafua mazingira kuacha tabia hiyo mara moja na badala yake sasa wawe tayari kujiunga na mfumo rasmi wa majitaka kutoka DAWASA ili kupunguza au kumaliza athari za kiafya na kimazingira zinazosababiahwa na tabia hiyo.

SASA
UNAWEZA
KUPIGA

181

NAMBA YA HUDUMA
KWA WATEJA DAWASA

BILA MALIPO